
Nipashe
Jumamosi Septemba 19, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580343
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya Dk. Mvungi

UKURASA 3




UKURASA 11

# AHADI ZAIDI



• **JPM** aahidi upanuzi Uwanja Kigoma, bandari mpya mbili, Lissu ataka ma-RC, ma-DC kupigiwa kura, mgombea urais ajinasibu mil. 1/- kila mjasiriamali, neema kwa walimu... *Endelea ukurasa.2*




Miili ya marehemu 10 ikiwa kwenye majeneza katika viwanja vya shule ya msingi Byamungu tayari kwa kufanyiwa Dua na Sala kabla ya kukabidhiwa kwa familia zao. **PICHA: ALLAWI KABOYO**

## IGP Sirro aula tena Polisi kimataifa

UKURASA 4

# Vilio vyatawala kuagwa miili wanafunzi walioungua moto

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE

# JPM aahidi neema zaidi Kigoma

**Na Gwamaka Alipipi,** KIGOMA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaahidi wananchi wa Mkoa wa Kigoma kuwa, atawafanyia mambo makubwa, ikiwa ni pamoja na kununua meli mbili mpya zitakazotatua kero ya usafiri Ziwa Tanganyika.

Vilevile, amewaahidi kufanya ukarabati wa meli ya Mv. Liemba, akibainisha kuwa tayari Sh. bilioni 10 zimeshatengwa pamoja na ukarabati wa meli ya Mv. Sangara iliyotengewa Sh. bilioni sita.

Akiwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma, jana Dk. Magufuli pia aliwahakikishia wakazi wa mkoa huo kuwajengea bandari mbili eneo la Kabwe na Kasanga, upanuzi wa uwanja wa ndege, ujenzi wa jengo la abiria na ghala la kuhifadhia mizigo.

Dk. Magufuli alisema: "Ninataka kuitengeneza Kigoma, ninataka kuifungua Kigoma, Nimechoka kusikia matukio ya ajali katika Ziwa Tanganyika."

Akifafanua zaidi ununuzi wa meli mpya, Dk. Magufuli alisema moja itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo na nyingine itakuwa inabeba mizigo tani 4,000.

Kuhusu ujenzi wa miundombinu ya barabara, Dk. Magufuli alisema Sh. bilioni 567 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara katika mkoa huo, zikiwamo barabara za Nyakanazi-Kibondo, Kidau-Kasulu na Kasulu-Namanyovu.

"Miaka minne iliyopita Kigoma ilikuwa imesahaulika, niliwahi kuja Kigoma nikiwa kidato cha pili, hakukuwa na usafiri, kulikuwa na treni tu, hakukuwa na barabara. Nilipoteuliwa kuwa rais, nikasema siwezi kuuacha Mkoa wa Kigoma, leo Kigoma inapendeza, lakini bado tunataka kuupanua zaidi mkoa huu kiuchumi.

"Wakazi wa Kigoma mkae mkao wa kufanya biashara, wauza dagaa, migebuka mtauza, huu ndiyo wakati wa kujipanga kimaendeleo. Makandarasi watakaoajiriwa kujenga barabara mkoani hapa wataajiri idadi kubwa ya watu, mama lishe watauza," alisema.

Dk. Magufuli pia alisema Mkoa wa Kigoma umewekwa katika mradi wa kuendeleza miji minane ya kimkakati (TSCD) inayojumuisha mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Tanga, Mtwara, kwamba serikali iliingia mkataba na Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kuendeleza baadhi ya miji katika mikoa hiyo.

"Waziri wa Fedha Dk. Philip Mpango, ndiye aliyetia saini mkataba huo, Sh. bilioni 799.52 zikitarajiwa kutumika kuendeleza miji minane ikiwamo mji wa Ujiji, Ilemela, Mikindani. Mtu akija akisema huu mradi ameuleta yeye maana yake mikoa yote hiyo nako alipeleka, tujiepushe na matapeli wa kisiasa," alionya.

Kuhusu zao la zao la michikichi, Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imefanikiwa kulifufua zao hilo baada ya kusahaulika.

Alisema aliwahi kumtuma Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, zaidi ya mara mbili kuzuru Kigoma kutatua kero za wakulima wa zao hilo.

Alisema mojawapo ya mkakati uliofanyika wa kuliinua zao hilo ni kufufua mashamba ya michikichi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

"Kuna watu wanajisifu eti wamefufua wao zao la chikichi, kwa hiyo nikimtuma mtu akifanya vizuri, watu wanajitokeza wanasema wamefanya wao," alisema Dk. Magufuli.

Kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika Mkoa wa Kigoma kwenye sekta ya afya kwa kipindi cha miaka mitano, Dk. Magufuli alisema: "Tumefanikiwa kujenga hospitali za wilaya Buhigwe, Kasulu, Uvinza. Vituo vya afya 10 tumejenga, 11 tumevikarabati.

"Tumejenga zahanati nne, 11 tumezikarabati, tumeleta dawa na vifaa tiba zenye thamani ya Sh. bilioni 18.27, utoaji wa chanjo kwa watoto umefanyika kwa asilimia 95, idadi ya wajawazito wanaojifungua katika vituo vya afya imeongezeka kutoka asilimia 55 mwaka 2015 hadi 98 mwaka jana," alisema.




Wanafunzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Don Bosco jijini Dar es Salaam, wakimsikiliza Mhariri wa Nipashe Wikiendi, Epson Luhwago, walipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya magazeti ya The Guardian Ltd, Mikocheni jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu: Ma-RC watapigiwa kura

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya CHADEMA, Tundu Lissu, amesema serikali yake itabadilisha utaratibu wa majimbo na kuruhusu wananchi kupiga kura kuwachagua wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi.

Lissu aliyasema hayo jana mjini Mpanda wakati akiendelea na kampeni zake za uchaguzi mkuu, akisema: "Kubadilisha utaratibu wa majimbo hatuna maana kuyarudisha majimbo ya kikoloni. Tutaweka utaratibu ambao mfano wananchi wa Mpanda au Katavi tukitaka mkuu wa mkoa, tunamchagua wenyewe, tukitaka mkuu wa wilaya, tunamchagua wenyewe."

Lissu alisema atahakikisha wananchi wakitaka fedha zao, ziwekwe chini ya mkurugenzi wa mji ambaye naye atachaguliwa na wananchi na akianza kuwanyanyasa wanamwondoa.

"Utaratibu wa leo ukoje? Fedha zote zinakwenda Dar es Salaam halafu wakikaa wanawarudishia vijisenti halafu mnashukuru Rais amewaletea maendeleo," alisema.

MIL.1/- KILA MJASIRIAMALI

Wakati Lissu akiahidi kufanya hayo, mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa, amesema kama wananchi watampa ridhaa, serikali yake itatoa mkopo wa Sh. milioni moja kwa kila mjasiriamali nchini.

Vilevile, amesema kila mwalimu atalipwa mshahara kuanzia Sh. milioni moja na kuendelea na kujengewa nyumba ya kuishi.

Mgombea huyo alisema jana kuwa fedha za mikopo kwa wajasiriamali bila dhamana badala yake dhamana itakuwa ni kitambulisho cha taifa.

Alisema katika kuhakikisha wajasiriamali wengi wananufaika na fedha hizo, serikali yake itaanzisha benki ya wajasiriamali badala ya benki ya biashara ambayo serikali inapeleka pesa huko na kuwatoza riba kubwa wakopeshwaji.

"Fedha watakazokopesha watazirudisha kwa kipindi cha miaka mitano na hazitakuwa na riba, tutaanza na wajasiriamali milioni moja ambapo zitatumika takriban Sh. trilioni moja kuwakopesha," alisema.

Aliongeza kuwa kila mwalimu atalipwa mshahara kuanzia Sh. milioni moja na atahakikisha walimu wote watajengewa nyumba za kuishi.

Alisema shule zote za mjini zitajengwa gorofa kuanzia mbili hadi tatu na ruzuku inayotolewa kwa vyama vya siasa, itapunguzwa kwa asilimia 30 ambayo itapelekwa kwenye vyombo vya habari ili kuboresha utendaji kazi wao.

Pia asilimia 30 itakwenda kwenye taasisi za dini lengo ni kwenda kuzisaidia taasisi hizo kuanzisha shule za watoto wenye maadili.

Alisema serikali yake pia itanunua ndege za gorofa ambazo zitatumika kuleta watalii nchini ambapo ndege zitafikia 30. Aliongeza kuwa ardhi itamilikiwa na wananchi badala ya sasa ambapo ardhi ni mali ya serikali.

***Imeandikwa na Romana Mallya na Thobias Mwanakatwe***

# CCM yakerwa na mabango kuchanwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, kimeelezwa kukerwa na baadhi ya wafuasi wa vyama vya upinzani wanaochana picha za wagombea ubunge na wa urais, Rais John Magufuli.

Kutokana na kuibuka kwa tabia hiyo, kimesema kimejipanga kuwachukulia hatua za kisheria na kuwafikisha mahakamani wataokamatwa kwa kuhusika na vitendo hivyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni wa chama hicho zilizofanyika mjini hapa, zilizohudhuriwa na wagombea ubunge katika majimbo yote. Mbunge wa zamani wa Kahama Mjini, James Lembeli pia alihudhuria mkutano huo.

Alisema limeibuka kundi la watu wanaochana mabango yenye picha za wagombea wa ubunge na urais kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa na kwamba atakayebainika au kukamatwa, atawajibishwa kisheria.

Magesa alisema huu muda si wa kuchaniana mabango yenye picha za wagombea, kutupiana mawe na kuvunjiana vioo vya magari na kuwataka wagombea wa vyama vingine kushindana kwa kunadi sera kupitia ilani zao kwa wananchi na kwamba kufanya hivyo ndiyo siasa safi.

"Vyama vingine vya siasa vimegeuka kuwa vya kuweka na kukopa. Vinapoishiwa sera za kuuza ilani ya vyama vyao kwa wananchi, vinaanza kuchana mabango, kurusha mawe na kuvunja vioo vya magari. Hatutakubali jambo hili na tutawachukulia hatua za kisheria wote wakaokamatwa wakichana mabango," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alisema mgombea urais wa chama hicho amefanya mambo makubwa hasa kwenye elimu.

Kwa Mkoa wa Shinyanga, alisema katika miaka mitano iliyopita zilitolewa Sh. bilioni 29.9 na watoto wanasoma bure sasa iweje mabango yachanwe.

Mlolwa aliwataka wananchi wa majimbo ya Kahama Mjini, Ushetu na Msalala kuhakikisha wanatunza shahada zao vyema na kupiga kura ifakapo Octoba 28, mwaka huu huku wakihakikisha wanachagua CCM katika ngazi za urais, ubunge na udiwani.

HABARI KITAIFA

## Majaliwa: Shule za Bariadi zimenufaika mfumo EP4R

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

SHULE 28 za Wilaya ya Bariadi (11 za msingi na 17 za sekondari), zimenufaika na mfumo wa uboreshaji wa miundombinu ya shule wa Lipa Kutokana na Matokeo (EP4R) uliotekelezwa tangu 2015 hadi 2020.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, aliyasema hayo jana alipozungumza na wakazi wa Kata ya Nkololo wilayani hapa kwenye mkutano wa kampeni.

Alisema awali zilitolewa Sh. bilioni 2.3 na Septemba mwaka huu zimetolewa Sh. milioni 457 ili kukamilisha uwekaji miundombinu ya nyumba za walimu, madarasa na matundu ya vyoo katika shule za msingi za Halawa, Kilabela A, Tunge, Mwauchumu, Bukiliguu, Byuna, Chungu cha bawawa, Damidami, Masewa C, Mwashagata na Banemhi za wilayani hapa.

"Kwa upande wa shule za sekondari, Sh. bilioni 1.07 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya nyumba za walimu, madarasa, maabara, majengo ya utawala na matundu ya vyoo kwa sekondari za Dutwa, Mwantimba, Gegedi, Miswaki, Mwamlapa, Nkololo, Nyasosi, Nyawa, Sapiwi, Banemhi, Gasuma, Igaganulwa, Ikinabushu, Itubukilo, Mwadobana, Sakwe na Nkindwabiye," alisema.

Kuhusu mpango wa elimu bila malipo, Majaliwa alisema shule za msingi 79 zilipatiwa Sh. bilioni 3.12 kwa ajili ya ukarabati wa majengo, masuala ya utawala, michezo, mitihani na posho kwa maofisa elimu kata na walimu wakuu.

Alisema shule za sekondari 23 zilipatiwa Sh. bilioni 1.43 kwa ajili ya kulipia fidia ya ada, chakula kwa shule za bweni na posho ya madaraka kwa wakuu wa shule.

Majaliwa alisema Sh. bilioni 3.2 zimetolewa kupitia TARURA kwa ajili ya matengenezo ya kawaida, matengenezo ya sehemu korofi, na ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km 246 ambazo zimefanyiwa matengenezo kwa kiwango cha udongo.

Alizitaja barabara zilizofanyiwa matengenezo hayo kuwa ni za Ikungulyabashashi – Ditima; Byuna - Nkindwabiye - Halawa; Igegu - Matongo Gibishi - Halawa; Dutwa-Gilya - Mwauchumu; Nyakabindi - Mwadobana - Gasuma; Kasori Centre - Kasori Ginnery na Nyamswa - Mwasubuya - Bwawani.

Mjumbe huyo wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa CCM, alitumia fursa hiyo kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, mgombea ubunge wa Bariadi, Kundo Mathew, mgombea udiwani wa Nkololo, Nyamwela Sinda na wagombea udiwani wa kata zote za wilaya ya Bariadi waliokuwapo kwenye mkutano huo.

# Vilio vyatawala kuagwa miili wanafunzi walioungua moto

**Na Allawi Kaboyo,** KYERWA

VILIO na majonzi jana vilitawala wakati wa kuagwa miili ya wanafunzi 10 waliokufa kwa ajali ya moto uliounguza bweni la wavulana katika Shule ya Msingi Byamungu, Kyerwa mkoani Kagera na kukabidhiwa kwa wanafamilia tayari kwa mazishi.

Miili hiyo iliagwa jana katika viwanja vya shule hiyo na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, kwa niaba ya Rais John Magufuli.

Akizungumza katika hadhara hiyo, Dk. Bashiru aliwapa pole wafiwa na wote walioguswa na msiba huo huku akiwasihi wafiwa kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo.

Dk. Bashiru pia aliitaka serikali na vyombo vya usalama kuendelea kufanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha moto huo. Pia aliiagiza serikali viongozi wa Mkoa wa Kagera kusimamia maagizo aliyoyatoa Rais Magufuli alipokuwa Bukoba na kuwataka wamiliki wa shule kuendelea kutoa ushirikiano pale watakapohitajika.

"Rais Magufuli ameniagiza nije hapa kuwapa pole kwa msiba huu mkubwa. Lakini ameniagiza pia kuweka msisitizo wa maagizo yake aliyoyatoa ya kuhakikisha mazingira ya watoto wetu wanapokuwa shuleni yanakuwa salama," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema serikali imekuwa bega kwa bega na wana Kyerwa, hasa wafiwa kwa kuhakikisha marehemu wanahifadhiwa vizuri pamoja na majeruhi wanatibiwa.

Gaguti alisema miili hiyo imekabidhiwa baada ya kukamilika kwa vipimo vya vinasaba (DNA) vilivyofanyika kwa lengo la kuwatambua watoto hao kutokana na kuungua vibaya.

"Serikali kwa kushirikiana na wazazi wa watoto hawa, tulifanya hivi makusudi ili kila mtoto atambulike na kuzikwa katika familia yake maana bila kusubiri DNA ilikuwa vigumu kuwatambua. Sasa wametambulika na wazazi angalau wamepata faraja kidogo kupata miili ya wapendwa wao" alisema.

Pia alisema tayari zimeundwa kamati za uchunguzi kwenye shule zote za bweni mkoani hapa kwa ajili ya kuangalia miundombinu.

Gaguti aliongeza kuwa kwenye msiba huo serikali imetoa gharama zote za mazishi ya wanafunzi waliofariki dunia ikiwamo kusafirisha miili pamoja na kuwahudumia majeruhi walioko hospitalini.

Sheikh wa Mkoa wa Kagera, Alhaj Kharuna Kichwabuta, alisema kuwa hali hii wanadamu wanatakiwa kuipokea kwa kuwa mpangaji wa kila ajali na tatizo kwa mwanadamu ni Mwenyezi Mungu.

Ajali hiyo ya moto uliosababisha vifo vya wanafunzi 10 na wengine kujeruhiwa, ilitokea usiku wa kuamkia Septemba 14, mwaka huu.



Mwenyekiti wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi Mashariki Mwa Afrika (EAPCCO) ambaye pia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini IGP Simon Sirro (Pichani), akifuatilia mkutano mkuu wa 22 wa mwaka uliofanyika kwa njia ya mtandao (video conference). Katika mkutano huo, IGP Sirro ameongezewa mwaka mmoja kuongoza Shirikisho hilo la Wakuu wa Polisi Mashariki Mwa Afrika. **PICHA: POLISI**

# Wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji ya Dk. Mvungi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imewahukumu washtakiwa watano kati ya sita kunyongwa mpaka kufa baada ya kukutwa na hatia ya kosa la kumuua kwa makusudi aliyekuwa Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Dk. Sengondo Mvungi.

Waliohukumiwa kunyongwa ni Msigwa Matonya, Mianda Mlewa, maarufu kama White, Paulo Mdonondo, Longishu Losingo na John Mayunga, maarufu kama 'Ngosha'. Hukumu hiyo ilitolewa na mahakama hiyo mbele ya Jaji Seif Kulita baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi 16 wa Jamhuri bila kuacha shaka imewaona washtakiwa watano kati ya sita wana hatia dhidi ya mauaji hayo.

Hata hivyo, ushahidi huo wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha kosa dhidi ya mshtakiwa Juma Kanungu, hivyo mahakama inamwachia huru.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi Cledo Lujagu, akisaidiana na Mawakili wa Serikali, Lilian Lwetabula na Veronica Mtafya.

"Bila kuacha shaka, mahakama yangu imeridhika na ushahidi wa Jamhuri ambao umethibitisha kwamba mshtakiwa wa kwanza, wa pili, wa tatu, wa nne na wa sita kwamba walimwua kwa makusudi Dk. Mvungi, watanyongwa mpaka kufa na mshtakiwa wa tano anaachiwa huru kwa kuwa hakuna ushahidi dhidi yake," alisema Jaji Kulika.

Aprili 6, 2017 washtakiwa hao walisomewa maelezo ya mashahidi kwa mara ya kwanza na Wakili wa Serikali Mwandamizi Patrick Mwita mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Ilidaiwa kuwa Ngosha alipofanyiwa upekuzi nyumbani kwake walikuta bastola ndogo aina ya Revolver, risasi 21 na baruti nne zilizokuwa ndani ya mfuko wa nailoni zilizofichwa ndani ya nyumba hiyo juu ya paa la nyumba pembeni.

Katika kesi ya msingi, washitakiwa hao kwa pamoja walikuwa wanakabiliwa na shtaka la mauaji ya Dk. Mvungi.

Ilidaiwa kuwa Novemba 3, 2013 walifanya kosa la mauaji ya kukusudia kinyume cha kifungu cha 196 cha Sheria na Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo ya tukio, katika eneo la Msakuzi Kibwegere, Wilaya ya Kinondoni (sasa Ubungo), washitakiwa hao kwa pamoja walimuua kwa kukusudia Dk. Sengondo Mvungi.

# Kortini madai kurusha maudhui bila leseni

**Na Hellen Mwango**

WATU wawili, akiwamo mwanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Isaya Massawe (22), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi mbili tofauti za kuchapisha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni.

Katika kesi ya kwanza, Massawe alisomewa shtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Ruboroga, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Adolf Ulaya alidai kuwa kati ya Februari 4, mwaka jana na Septemba 16, mwaka huu, mahali tofauti jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alitenda kosa hilo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo alichapisha maudhui mtandaoni kupitia channel ya YouTube yenye jina la Isaya Thomas Massawe, bila kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mshitakiwa baada ya kusomewa shitaka hilo, alikana na upande wa mashitaka ulidai upelelezi wa shauri hilo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Ruboroga, alimtaka mshtakiwa kutimiza masharti ya kuwa na wadhamini wawili waaminifu watakaotia saini dhamana ya Sh. milioni tatu kila mmoja.

Mshitakiwa alitimiza masharti ya dhamana na yuko. kesi itatajwa Oktoba 15, mwaka huu.

Katika kesi ya pili, anayedaiwa kuwa Ofisa Habari Msaidizi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, (CHADEMA), Dominic Mgaya, alisomewa shtaka la kurusha maudhui mtandaoni bila kuwa na leseni.

Mgaya alisomewa shtaka lake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate huku Wakili wa Serikali, Adolph Ulaya, akidai kuwa mshitakiwa alitenda kosa hilo kati ya Oktoba 14, 2017 mpaka Septemba Mosi, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alirusha maudhui hayo kupitia chaneli ya Youtube iitwayo Chadema Media TV bia kuwa na leseni kutoka TCRA.

Baada ya kusomewa shitaka hilo, mshtakiwa huyo alikana, upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa ambapo ilipangwa Oktoba 20, mwaka huu.

Mshtakiwa huyo aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza sharti la kuwa na wadhamini waliotia saini bondi ya Sh. 500,000 kila mmoja.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Donatus Richard (kushoto) pamoja na walimu wa Shule ya Msingi Twiga iliyopo wilayani humo jijini Dar es Salaam, wakishangilia baada ya Benki ya NMB kukabidhi Meza na Viti vyenye thamani ya Sh. milioni tano kwa ajili ya walimu wa Shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# IGP Sirro aula tena polisi kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Wakuu wa Polisi Mashariki Mwa Afrika (EAPCCO) wamemtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro (pichani), kuendelea kuwa mwenyekiti wake kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja.

Kutokana na ombi hilo, IGP Sirro amekubali kuendelea kutekeleza jukumu hilo huku akielezea mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka mmoja aliokuwa madarakani.

Uamuzi huo ulitolewa jana na nchi 14 wanachama wa shirikisho hilo kupitia mkutano wake mkuu wa 22 wa mwaka uliofanyika kwa njia ya mtandao (video conference).

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi nchini ilisema jana kuwa Sirro amekubali ombi hilo huku akibainisha kuwa shirikisho hilo limepata mafanikio makubwa.

Pia Sirro alikaririwa akisema kwa katika kipindi cha mwaka 2020/21 wamejipanga kutekeleza yale ambayo hayakufikiwa na watahakikisha kuwa nchi wanachama zinabadilishana uzoefu na kufanya mafunzo ya pamoja ya mbinu za medani.

Aidha, katika kikao chake na waandishi wa habari jijini Dodoma, IGP Sirro alisema ushirikiano na wakuu wa polisi Mashariki Mwa Afrika umewezesha kudhibiti uhalifu wa kupanga na unaovuka mipaka.

IGP Sirro aliyataja mafanikio mengine kuwa ni udhibiti wa usafirishaji wa nyara za serikali sambamba na kudhibiti biashara haramu ya usafirishaji binadamu na dawa za kulevya.



IGP Sirro anaendelea tena kuongoza shirikisho hilo kwa kipindi kingine cha mwaka mmoja tangu pale alipochaguliwa katika mkutano mkuu wa 21 wa mwaka uliofanyika mwezi Septemba mwaka jana jijini Arusha.

# GGML yadhamini maonyesho ya madini kwa mil. 200/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imedhamini Maonyesho ya Tatu ya Teknolojia za Uchimbaji Madini mkoani Geita kwa gharama ya Sh.milioni 200.

Maonyesho hayo yalianza juzi hadi Septemba 27, mwaka huu, huku GGML ikiwa mdhamini mkuu.

Udhamini huo unahusisha gharama za kusawazisha eneo la maonyesho pamoja na kugharamia mabanda 100 pamoja na umeme wa dharura (jenereta na mafuta yake) katika kipindi chote cha maonyesho hayo.

Maonyesho hayo ambayo yanafanyika katika viwanja vya Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji na Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) Mjini Geita ambalo pia limejengwa na Kampuni ya GGML kupitia mpango wake wa huduma kwa jamii kwa gharama za Sh. milioni 800.

"GGML inajivunia kudhamini maonyesho haya kwa mwaka wa tatu mfululizo. Mwaka huu tunakusudia kutoa uzoefu wetu wa matumizi ya vifaa mbalimbali vya uchimbaji kwa kampuni nyengine, lakini pia kwa wachimbaji wadogo. Ni jambo zuri pia kwamba tumetoa udhamini huu tukiwa tunaadhimisha miaka 20 ya uwekezaji wetu mkoani Geita na Tanzania. Tunajivunia kuendeleza ushirikiano na jamii inayotuzunguka kunufaisha wafanyabiashara wa ndani wanaokusudia kufanya kazi na sisi," alisema Simon Shayo, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu.

"Tunafarijika sana kuona ndoto ya kuwa na kituo cha uwekezaji na biashara ya nje hapa Geita inatimia na GGML inakuwa sehemu ya mafanikio hayo kupitia mpango wake wa kusaidia jamii," alisema.

Maonyesho haya yanakutanisha kampuni za uchimbaji madini, wachimbaji wadogo na wa kati, wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Tanzania na nchi nyingine kwa ajili ya kuonyesha teknolojia zinazotumika katika sekta ya uchimbaji madini na fursa za uwekezaji na biashara kwenye sekta hiyo.

Mwaka 2019, Kamati ya Maandalizi ya Maonyesho ya Teknolojia za Uchimbaji Madini, iliitunukia GGML tuzo ya mshindi wa kwanza aliyetoa elimu na mafunzo ya teknolojia muhimu kwa wachimbaji wadogo sanjari na mifumo ya usalama na uokoaji inayopaswa kutumika migodini.

**Tunafarijika sana kuona ndoto ya kuwa na kituo cha uwekezaji na biashara ya nje hapa Geita inatimia na GGML inakuwa sehemu ya mafanikio hayo kupitia mpango wake wa kusaidia jamii.**

HABARI KITAIFA

# Bil. 3.7/- zatumika miradi maji Busega

**Na Wandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amesema Sh. bilioni 3.7 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika Wilaya ya Busega.

Majaliwa alisema hayo jana kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata za Mkula na Lamadi, Busega mkoani Simiyu akiwa njiani kwenda Bunda, mkoani Mara.

Alisema fedha hizo zimetumika kujenga mradi wa bomba la maji katika kijiji cha Lukungu ambao tayari umekamilika.

"Pia fedha hizo zilitumika kufanya ukarabati wa chanzo cha maji katika mradi wa maji wa Kalemela-Mkula ambao nao tayari umekamilika," alisema.

Ameitaja miradi mingine kuwa ni wa maji bomba Kiloleli unaohudumia vijiji vya Ihale, Ijitu na Yitwimila B ambao pia umekamilika.

Kwa mujibu wa Majaliwa, fedha hizo zimetumika kufanya upanuzi wa mradi wa maji Lamadi (Kalago na Mwabayanda) ambao umefikia asilimia 50; upanuzi wa mradi wa maji Nyashimo ambao umefikia asilimia 10; ujenzi wa mradi wa maji Mkula Sekondari ambao umefikia asilimia 60 na wa maji Bushgwamhala ambao umefikia asilimia 100.

Kuhusu umeme, Majaliwa alisema kati ya vijiji 59, vijiji 53 vimeshapelekewa huduma ya umeme, na vijiji sita bado havina umeme. Alisema vijiji ambavyo havina umeme, viko kwenye mpango wa kupelekewa umeme

Wakati huohuo, Majaliwa alisema ili kuboresha miundombinu ya barabara katika wilaya hiyo mpya, Sh. bilioni 2.3 zimetolewa kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika miaka mitano iliyopita.

Alisema fedha zilizotolewa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara zilihusisha barabara za Mwamanyili – Busami; Shule ya Sekondari Masanza - Sayaka Road; Nyamikoma - Busega na Lamadi Sekondari - Suti Moja.

Alizitaja barabara zingine kuwa ni Masanja- Ashico Petrol Road; Malili- Mwamigongwa- Ng'wang'wenge; Nyang'haya- Kasoli na Ngong'ho- Ndono Petrol Station.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais John Magufuli, mgombea ubunge wa jimbo la Busega, Simon Songe na wagombea udiwani wa kata zote za Busega.

# Mkuu JKT atoa neno kuhusu uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Charles Mbuge, amewataka Watanzania kusikiliza sera za wagombea wa uchaguzi mkuu na kuchagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo na si kudumaza.

Sambamba na hilo, amesema jeshi hilo si sehemu ya kutafuta ajira bali ni kufundisha vijana stadi ambazo watatumia kwenye maisha yao.

Jenerali Mbuge aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya awali ya Operesheni Uchumi wa Kati 2020 kwa watumishi 41 wa Bunge ambayo yalianza Agosti 17 na kuhitimishwa jana katika Kikosi cha JKT Makutupora.

Aliwataka wananchi kupata muda wa kusikiliza sera za wagombea na kuchagua viongozi bora watakaosaidia nchi kuendelea kufanikiwa kimaendeleo na si kudumaza maendeleo.

"Nendeni mkasikilize hoja za wagombea wote na kuzipima ili ikifika Oktoba 28 mwende kuchagua kwa kuangalia pumba na mchele, mkachague viongozi wa kuifanya Tanzania iwe salama," alisema.

Kuhusu mafunzo hayo, kiongozi huyo aliwataka wahitimu kutanguliza mbele maslahi ya taifa na kuwa viongozi bora kwenye maeneo yao na kuhakikisha vikwazo wanavyokumbana navyo vinakuwa fursa kwao na si kudhoofisha utendaji kazi.

Pia aliwasihi kufanya kazi zao kwa kuzingatia kiapo chao wakati wa kutekeleza majukumu yao.

"Ni vyema watumishi mkirudi kwenye majukumu yenu mkatekeleze kwa kuzingatia kiapo chenu na kuwa viongozi bora wa mfano na wa kuigwa. Mmejifunza mengi kwenye mafunzo haya mnapaswa kuyazingania wakati wa kufanya kazi na kuzingatia kiapo chenu," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka kuwa tayari muda wote kulitumikia taifa ndani na nje ya nchi kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa kwa kuwa wao wamekuwa jeshi la akiba.

Kaimu Kamanda wa Kikosi cha JKT Makutupora, Luteni Kanali Festo Mbanga alisisitiza kuwa watumishi hao wawe mfano mzuri wa kufanya kazi kwa bidii na kwa uzalendo kulingana na waliyojifunza.

Naye Kaimu Mkuu wa Tawi la Mafunzo JKT, Kanali Amos Mollo, aliwataka wahitimu hao kuwa mabalozi kwa watumishi wenzao na kuzingatia utendaji wenye tija.

Akisoma risala ya wahitimu hao, Nemelwa Mwihambi, alishukuru uongozi wa bunge na jeshi kwa kuwapatia mafunzo hayo kwa kuwa wamejifunza nidhamu, utii na uhodari katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mwihambi aliomba mafunzo hayo yawe endelevu kwa kujumuisha watumishi wa taasisi na mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi na kuitumikia nchi kwa uadilifu.



Mgombea wa ubunge jimbo la Rufiji mkoani Pwani kwa tiketi ya CCM, Mohamed Mchengerwa (katikati), akielekea kwenye kampeni zake jana eneo la Ikwiriri kwa usafiri wa bodaboda. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mgombea wa ubunge ataja mbinu kumaliza kero maji

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, amewaahidi wananchi kuwa, kama watampa ridhaa atajenga mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Nyasa na mito inayozunguka wilaya ili kukabiliana na ukosefu wa maji safi na salama.

Akizungumza juzi na wananchi wa kata ya Makwale kwenye mkutano wa kampeni, alisema upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa wilaya ya Kyela umekuwa ni kero ya muda mrefu ambayo haijapatiwa ufumbuzi.

Mwalwage alisema hakuna sababu yoyote ya msingi kwa Kyela kukosa huduma ya maji safi na salama wakati kuna Ziwa Nyasa na zaidi ya mito minne ambayo inazunguka wilaya hiyo.

Alisema inawezekana kabisa kujenga mradi mkubwa wa maji ambapo maji yanaweza kuchukuliwa kutoka Ziwa Nyasa na kuyasambaza kwa wananchi wote wa jimbo, kazi ambayo ataifanya mara tu baada ya kuingia bungeni.

"Serikali ya CCM inasema kiwango cha upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kyela ni asilimia 68.92 hadi 73.17 ya wakazi wote wa mjini na vijiji lakini ukweli ni kwamba kiwango cha upatikani wa maji ni chini ya asilimia 30," alisema.

Mwalwage alisema mbunge aliyetangulia Dk. Harrison Mwakyembe, alifanya kazi nzuri kwa kusaidia kuchimbwa visima vya maji lakini bahati mbaya vingi havifanyi kazi.

Aliongeza kuwa kukosekana kwa maji safi na salama kumekuwa kisababishi cha magonjwa ya tumbo na kichocho na mengineyo na kusababisha wananchi kutumia gharama zisizostahili kwa ajili ya matibabu. Kuhusu kilimo, alisema wakulima wa mpunga ambalo ndilo zao kuu la biashara katika Wilaya hiyo wanapata tabu kutokana na kutozwa ushuru mkubwa na hivyo kuwafanya washindwe kunufaika na kilimo hicho.

Alisema akiingia bungeni atakwenda kuishinikiza serikali ifute kabisa ushuru wa mazao kwa wakulima wa mpunga ili kilimo hicho kiweze kuwanufaisha na hivyo kuboresha maisha yao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba SC, Namungo msisahau maandalizi michuano ya CAF

**WAKATI** raundi ya tatu ya mechi za Ligi Kuu ikiendelea wikendi hii na vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga wakifunikwa na KMC, Dodoma Jiji FC na Azam FC zinazoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo, ni wakati mwingine wa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa kuanza pia kujipanga.

Mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ndio michuano mikubwa kwa ngazi ya klabu hapa barani.

Timu hizo zitaanza kusaka ufalme huo wa Afrika mapema Novemba, mwaka huu, na mechi za Ligi Kuu Bara zikiwa ni sehemu kubwa ya kuwaandaa wachezaji wao kikamilifu.

Wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano hayo kwa mwaka huu ni Simba ya jijini Dar es Salaam itakayoshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na huku Namungo kutoka mkoani Lindi ikitarajiwa kwenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Mbali ya klabu hizo kuhitaji kufanya vizuri katika mechi zake za Ligi Kuu Tanzania Bara, benchi la ufundi na wachezaji wanatakiwa kuweka katika mipango yao namna watakavyopambana kuhakikisha wanafanya vema kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Nipashe inawakumbusha Simba na Namungo, kwa sababu ingependa kuona klabu hizo ambazo zilifanya vizuri katika msimu uliopita, zinafika mbali na hivyo kulitangaza vema jina la Tanzania na si kuwa washiriki.

Tanzania haikuwa na matokeo mazuri katika msimu uliopita wa mashindano hayo ya CAF, baada ya timu zake kushindwa kufika kwenye hatua ya makundi, na kuipoteza nafasi ya kutoa klabu nne katika michuano hiyo kama ilivyopata mwaka juzi.

Matokeo mazuri yanatokana na maandalizi sahihi, hii inamaanisha mchezo wa soka unahitaji maandalizi ya kiwango cha juu na kamwe hakuna miujiza katika kusaka ushindi au mafanikio.

Mbali na kila timu kujipanga kushinda kwenye mechi za nyumbani, wachezaji wanatakiwa kuandaliwa kupambana pia wanapokuwa ugenini kwa sababu katika mpira wa miguu, hakuna kinachoshindikana kama kila mmoja atatimiza majukumu yake.

Tunawakumbusha wadau wetu hasa Simba na Namungo, mafanikio ya timu hutokana na nguvu kazi ya pamoja, wachezaji hawatakiwi kuchanganya changamoto za nje ya uwanja wanapokuwa dimbani wakipambana kusaka ushindi.


Ili kufikia malengo, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linatakiwa kufanya mawasiliano na wawakilishi hao ili kujua kwa karibu wanavyojiandaa na michuano hiyo, kwa sababu kufanya vema kwa klabu hizo, ni sifa pia kwa shirikisho hilo.

Tumeliweka hili wazi kwa sababu timu kama Namungo ni ngeni katika mashindano ya kimataifa, hivyo viongozi wake wasione aibu kukutana na maofisa wa TFF katika kujifunza na kupata 'madini' ili malengo ya kufanya vizuri yafikiwe.

Tunashuhudia timu kongwe zikifanya makosa ya kikanuni kila simu ambayo huwagharibu kwa kupokonywa pointi au kutakiwa kulipa faini, ili haya yasijitokeze, ni vema Simba na Namungo zikajiandaa vizuri na mashindano hayo ya kimataifa ambayo yako mbioni kuanza.

Tayari ratiba ya Ligi Kuu Bara imeshatoka, lakini pale itakapowezekana 'kuichekesha' kwa maslahi ya Taifa, TFF isisite kufanya hivyo kwa sababu ya kuzingatia jiografia ya Tanzania, ambapo baadhi ya mechi huchezwa kwenye mikoa ambayo haina viwanja vya ndege na kulazimika kutumia usafiri wa barabara.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kila ngoma ina mchezo wake

Na Barnabas Maro

**KILA** ngoma huwa na namna yake ya kuchezwa. Maana yake kila jambo huwa na mbinu au taratibu zake za kulifanya. 'Ngoma' ni ala ya muziki iliyotengenezwa kwa ngozi iliyowambwa kwenye mduara wa pipa au mzinga; mchezo wa kutikisa mwili na kunengua unaofuata mdundo wa ala ya muziki.

'Mchezo' ni jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi; jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Kwa mfano, mchezo wa kandanda/kabumbu hupendwa sana duniani.

Simba na Yanga zipambanapo, Tanzania nzima zikiwamo nchi jirani hufuatilia kwa makini runinga na redio. Baadhi ya watu huwekeana madau, yaani fedha au vitu wanavyoahidiana kutoka kwa anayeshinda. Ni aina fulani ya kamari.

Nilipokuwa naandaa makala yangu, timu ya Mbeya City ilikuwa katika nafasi ya mwisho kati ya timu 18 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara. Timu hiyo ilikuwa imecheza michezo miwili na kupoteza yote. Kwanza ilifungwa mabao 4-0 na KMC halafu ikafungwa bao 1-0 na Yanga, mechi zote zikichezwa jijini, Dar es Salaam.

Mpaka sasa najiuliza ilikuwaje Mbeya City kufungwa mabao 4-0 na KMC lakini ikafungwa bao 1-0 kwa mbinde ilipocheza na Yanga yenye wachezaji wengi wa kimataifa? Muda wote Mbeya City ilipocheza dhidi ya Yanga, niliwaza na kuwazua ilikuwaje timu hiyo kufungwa idadi kubwa ya magoli na KMC kwa namna ilivyoisumbua Yanga?

Kuna wakati niliacha kuangalia mchezo ule kwa wasiwasi nikihofia Yanga kufungwa nyumbani. Niliposikia nderemo mitaani nilikimbilia ukumbini kuangalia runinga na kujua Yanga ilipata bao zikiwa zimesalia dakika chache mno mchezo umalizike! Nikajisemea kimoyomoyo 'Alhamdulillahi' (tamko la kuonyesha shukurani kwa Mwenyezi Mungu.) Mtu na chake Bwana!

Nadhani msimu huu kila timu itakuwa imejiandaa vizuri. Kwa hiyo timu zinazoitwa 'kubwa' zapaswa kuwa makini, hasa kwa timu ngeni zinazoshiriki Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu.

Mpaka nilipokuwa naandika makala (tarehe 16/9/2020), timu zote 18 zilikuwa zimecheza mechi mbili kila moja. KMC, Azam FC, Dodoma Jiji na Biashara United zilikuwa zikiongoza kwa alama sita kila moja. Simba na Yanga zilifuatia zikiwa na alama 4 kila moja.

Kinachofurahisha ni timu ngeni zinazoshiriki Ligi Kuu msimu huu, Dodoma Jiji, Ihefu na Gwambina, mpaka wakati naandika makala yangu zilionyesha kujiandaa vya kutosha, hivyo kuwa tishio kwa timu zingine wakiwamo wapinzani wa jadi, yaani Simba na Yanga. Ni nafasi nzuri kwa timu ngeni kuzichachafya klabu zinazodhani kuwa ndizo 'bora' kumbe kila chenye mwanzo kina mwisho wake.

Wahenga walisema "Hakuna kubwa lisiloshindwa." Maana yake hakuna jambo lisilowezekana. Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayekabiliana na hali ngumu kuwa hatimaye atafanikiwa. Aidha, ilisemwa "Vita havina macho." Maana yake vita havioni; hivyo huweza kumdhuru yeyote.

Hebu niwazindue waamuzi au marefa ambao waamuzi wa mchezo kama vile kandanda, mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa sheria za mchezo zinafuatwa na kuwaadhibu wasiozifuata. Anapaswa kuwa makini sana na kuhakikisha anafuata sheria 17 za mchezo wa kandanda bila upendeleo ama wa kuitetea timu aipendayo.Ingawa baadhi ya waamuzi wana timu wanazozipenda, wanapaswa kutumia haki bila upendeleo katika kutekeleza majukumu yao.

Kadhalika kuna viongozi wa vilabu wenye tabia ya kuwahonga marefa ili timu zao zishinde wakidhani ndio maendeleo! Sio kuwa wanajidanganya tu, bali pia wanaharibu maendeleo ya wachezaji na mwisho kuifanya nchi kutokuwa na wachezaji mahiri wenye nidhamu ya mchezo huo. Wahenga walisema: "Atupaye tope hujichafua mwenyewe." Maana yake mtu anayetupa au anayerusha tope hujichafua mwenyewe.

"Aulizaye humshinda asiyeuliza." Maana yake anayeuliza huwa amemshinda asiyeuliza kwa kuwa hujifunza. Twafunzwa tusione haya kuuliza mambo tusiyoyajua. Hivi Tanzania ina marefarii wangapi wa FIFA wanaochezesha mechi za kimataifa?

Zamani tulikuwa na mwamuzi mwenye asili ya Mkoa wa Kagera aliyeitwa Gratian Matovu aliyestaafu na kufariki Februari 3, mwaka 2012 jijini Dar es Salaam. Alikuwa mwamuzi wa kimataifa ambaye Tanzania ilijivunia kuwa naye. Huyu ndiye aliyezichezesha Simba na Yanga wakati Wekundu wa Msimbazi walipoibugiza Yanga mabao 6-0.

Kama tunaye refa mwanadada aitwaye Jonesia Rukyaa pia kutoka Mkoa wa Kagera aliyeibuka hivi karibuni, wako wapi wengine? Au Mkoa wa Kagera ndio pekee wenye watu wanaomudu kuwa waamuzi wa kimataifa? Waliomtangulia wako wapi na kinachowashinda kuwa kama marehemu Matovu na mwanadada huyo ni nini?

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# Bila NIDA, pasipoti hakuna huduma malazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAGENI wa ndani na nje ya nchi watakaolala kwenye hoteli na nyumba za kulala wageni zilizosajiliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mujibu wa sheria, kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu, watatakiwa kuanza kusajiliwa kwenye mfumo wa kielektoniki wa MNRT Portal.

Katika kutekeleza sheria hiyo, wageni hao watatakiwa kuwa na vitambulisho vya taifa (NIDA) au hati za kusafiria. Kwa wale ambao hawatakuwa na vitambulisho hivyo, watasajiliwa kupitia namba za simu au leseni za udereva.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi wa Utalii, Philip Chitaunga, alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja ya usajili wageni wanaolala kwenye huduma za malazi kupitia mfumo wa kielektoniki wa MNRT Portal kwa wamiliki wa malazi wapatao 200 wa Kanda ya Pwani.

Alisema lengo kuu la kusajili wageni katika huduma hizo ni kupata taarifa zitakazosaidia serikali kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kuboresha sekta ya utalii nchini.

Kwa mujibu wa Chitaunga, taarifa hizo zitatumika kama nyezo katika kuandaa sera, mikakati na mbinu katika kuboresha sekta ya utalii hasa utalii wa ndani ambao mwamko wake umekuwa mdogo.

Mfumo huo wa kusajili wageni, alisema utatumika katika hoteli, lambi pamoja loji pekee zinazotambulika na wizara hiyo.

Alisema utaratibu huo wa kusajili wageni ni takwa la kisheria, hivyo akawataka wamiliki wa malazi kuhakikisha kuanzia Oktoba Mosi, wanaanza kutekeleza agizo hilo kwa kusajili wageni wanaofika katika huduma za malazi kwa kutumia vitambulisho hivyo.

Katika hatua nyingine, Chitaunga amewatoa hofu wamiliki wa malazi kuwa taarifa hizo za wageni zitatumika kwa ni kwa ajili ya matumizi ya serikali pekee na zitatunzwa kwa usiri wa hali ya juu.

Samson Nelsa, mmiliki wa huduma za malazi katika Mkoa wa Pwani, alisema mfumo huo utasaidia serikali kuandaa takwimu za watalii

Alisema mbali na kuisaidia serikali kupata takwimu za utalii wa ndani na wa nje, pia utasaidia wamiliki wa hoteli kuwa na sehemu salama ya kuhifadhia taarifa zao.

Naye Mohamed Juma, mmiliki wa hoteli ya Rainbow, licha ya kuipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kutaka kujua takwimu halisi ya watalii kupitia mfumo huo, aliiomba wizara kuhakikisha hakuna taarifa za wateja zinatumika kwa ajili ya maslahi binafsi.

Aidha, aliitahadharisha wizara kuwa makini katika kuulinda mfumo ili usishambuliwe na baadhi ya watu wenye maslahi yao binafsi.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Mary Maganga (katikati) akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi rasmi wa mpango mkuu wa maendeleo wa sekta ya fedha kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia 2019 /20 hadi 2029/30 uliozinduliwa jana Jijini Dodoma ,kulia ni mwakilishi kutoka Wizara ya fedha Zanzibar, Hamisi Mwalimu na kushoto ni Kamishna Wizara hiyo,Charles Mwamaja. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## TASAC yajizatiti kuboresha huduma

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limesema litaendelea kuweka mazingira rafiki ya usafirishaji na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi bila kuingiliana na taasisi zingine.

Pia limesema litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuepuka mgongano wa kimaslahi na upande wowote.

Mkurugenzi Mkuu wa TASAC, Emmanuel Ndomba, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari.

Ndomba alisema lengo la TASAC si kuua taasisi zingine bali ni kushirikiana nazo katika kufanikisha utoaji wa huduma bora zaidi.

"TASAC ipo kwa mujibu wa sheria, utendaji wake pamoja na utoaji wa huduma hauingiliani na taasisi nyingine," alisema Ndomba.

"Tuna wataalamu wenye weledi na katika kipindi kifupi cha utendaji wetu huu wa mwaka mmoja, tumefanya maendeleo mengi na tunaamini tutaendelea kuleta mageuzi makubwa zaidi," aliongeza

Ndomba alisema kwa sasa wanaendesha shughuli zake kisasa zaidi tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma.

"Katika upokeaji wa meli, sisi tumeweka mifumo ambayo inatusaidia kuzipokea kwa njia za kisasa zaidi, lazima tufanye kazi kulingana na mabadiliko ya teknolojia, na tunahakikisha kwamba shughuli zetu haziingiliani na majukumu ya taasisi zingine," alisema Ndomba.

Pia alisema kwa sasa gharama wanazotoza katika usafirishaji wa makontena ni ndogo kulinganisha na ile iliyokuwa ikitozwa katika miaka ya nyuma na kwamba lengo ni kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara.

# Taasisi kuonyesha fursa waliohitimu masomo nje

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za serikali zimepongeza Global Education Link (GEL) kwa kuwaunganisha vijana Watanzania kusomea taaluma mbalimbali zikiwamo zile adimu nje ya nchi hivyo kuzalisha wataalamu kwenye fani nyeti zilizokuwa na uhaba wa wataalamu.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) .

Taasisi hizo pia zimeahidi kushiriki kwenye mahafali ya pili ya kimataifa yaliyoandaliwa na GEL yatakayofanyika leo Mlimani City, jijini Dar es Salaam, ambapo zitawaonyesha wanafunzi hao fursa mbalimbali za mafunzo na ajira walizo nazo.

Ahmed Abdi, Mkufunzi waa NIT alisema mahitaji rasilimali watu ni makubwa kutokana na fani ya usafiri wa anga kuendelea kukua mwaka hadi mwaka, hivyo wanahitaji walimu kwa ajili ya mafunzo katika vyuo.

Mkufunzi huyo alisema ajira zipo katika fani ya usafiri wa anga kwa kuwa ni fani ni pana tofauti na fikra za baadhi ya watu kwamba inahusu kurusha ndege tu.

Alisema kwenye fani hiyo, kuna waongoza ndege, wanaohudumia ndani ya ndege, watu wa usalama na kuhudumia ndege inapotua, hivyo ina mambo mengi na si kurusha ndege tu.

Naye Mkuu wa Rasilimali Watu na Utawala wa ATCL, Lembris Laanyuni, alisema watashiriki kwenye maonyesho katika mahafali ya 19 kama wadau kukutana na wanafunzi ili kujua wanaweza kupata fursa gani ndani ya shirika hilo.

"Tutakuwepo kwenye mahafali na tutakuwa na banda letu tutawaelezea kazi zetu na fursa zilizopo wale wenye hamu ya kwenda kusome usafiri wa anga na wale wenye maswali kuhusu masuala ya anga watembelee banda letu siku ya mahafali tunawaeleza fursa mbalimbali zinazotokana na uwapo wa shirika hili," alisema.

Daktari Bingwa wa Moyo wa JKCI, Dk. Tulizo Sanga, alisema maradhi ya moyo ni mengi na kuna uhaba mkubwa wa madaktari bingwa wa magonjwa hayo wakiwemo wauguzi waliobobea kwenye moyo.

Pia alisema wana uhaba wa wataalamu wa teknolojia na wataalamu wa usingizi kwani waliopo sasa nchi nzima ni wachache sana hawatoshelezi kulinganisha na idadi ya watu.

"Wataalamu wa mfumo wa umeme wa moyo nao ni wachache sana nashukuru serikali mtambo mwingine utafungwa kuwapima na kuwafanyia matibabu wagonjwa wenye shida ya mifumo ya umeme wa moyo tunasomesha watu wetu ingawa bado wachache sana," alisema.

# CCM Kahama watangaza kuvunja makundi

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

WANACHAMA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), waliotia nia ya kugombea ubunge katika jimbo la Kahama Mjini, wametangaza kuvunja makundi na kumuunga mkono Jumanne Kishimba.

Wakizungumza wakati wa kufungua kampeni za ubunge na udiwani katika jimbo la Kahama Mjini juzi, baadhi ya watiania hao wameomba makundi yote yaliyokuwapo wakati wa kura za maoni, sasa yamuunge mkono mgombea huyo.

Mbunge wa zamani wa jimbo hilo, Jemes Lembeli, ambaye katika kura za maoni alishika nafasi ya tatu, alisema ili kupata ushindi wa kushindo kwa wagombea wa CCM, lazima wanachama wote wawe wamoja na kukubali kumpigania mgombea aliyepitishwa na chama.

Nao Benjamini Ngaiwa na Godfrey Ihema, walisema Kishimba ndiye anayeweza kuwawakilisha wananchi wa Kahama katika nafasi ya ubunge, hivyo hakuna haja ya kuendeleza makundi.

Kwa upande wake, Kishimba alisema iwapo wananchi watampa ridhaa ya kuongoza tena kwa miaka mitano, atahakikisha anamshauri Rais apandishe kodi katika unga wa ngano ili wakulima wapate soko la uhakika.

Awali, mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, aliwataka wanachama wa chama hicho, kuendelea kuwaamini wagombea kwa kuwa wana uwezo wa kutekeleza sera zenye maendeleo kwa wananchi.




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhandisi Robert Gabriel (katikati) akizungumza na wajasiliamali pamoja na wachimbaji wadogo (hawapo pichani), wakati akizundua mafunzo maalumu ya siku tatu kwa wajasiliamali hao yanayofanyika kwenye maonesho ya dhahabu na teknolojia yanayofanyika mkoani humo yakilenga Mafunzo kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara zao kwa ufanisi na kwa viwango shindani vya kimataifa. Wengine ni pamoja na Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje. **MPIGAPICHA WETU**

# RC awa mbogo wasiojali wafanyakazi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amewataka wamiliki wa viwanda ndani ya mkoa huo kuzingatia haki na maslahi ya wafanyakazi wao.

Ndikilo alitoa rai hiyo jana alipotembelea kiwanda cha kuunganisha magari kilichoko eneo la TAMCO, mjini hapa.

Alisema ajira zinazotolewa kwa wafanyakazi zinatakiwa kuendana na haki vikiwamo vitendea kazi, maslahi na afya zao wakiwa kazini.

"Baadhi ya wamiliki hawazingatii haki na maslahi ya wafanyakazi wao. Wanawajali pale wanapokuwa wazima na kufanya kazi kwa bidii lakini wakipata matatizo hawana habari nao. Niwaombe waajiri kuheshimu wafanyakazi na kuwajali muda wote wakiwa kazini na wanapokumbana na matatizo," alisema Ndikilo.

Mkuu huyo wa Mkoa pia aliwataka wamiliki wa viwanda kutumia benki zilizopo ndani ya mkoa kupitisha fedha zao na kuomba mikopo, ili kukuza pato la mkoa na taifa kwa ujumla.

Sambamba na hilo, alizitaka taasisi wezeshi za mkoa huo kujipanga vizuri kutoa vibali kwa wawekezaji ili shughuli za uwekezaji zifanyike kwa wakati.

Awali, Meneja wa Kiwanda hicho, Ezra Mereng, alisema kiwanda hicho cha magari kitakapokamilika kitakuwa na uwekezaji wa zaidi ya Sh. bilioni 12.

Aliongeza malengo yao ya baadae ni kuwa na ajira 300 za moja kwa moja na zisizo rasmi 700 na kwamba kwa sasa zipo ajira 65 pekee.

## Makandarasi wavivu watangaziwa kibano

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

WAKALA wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) katika Halmashauri ya Mji wa Kahama, imesema katika mwaka wa fedha wa 2020/21, haitatoa tenda yoyote kwa makandarasi wavivu wanaotekeleza miradi kwa kusuasua.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Meneja wa TARURA wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Job Mtagwaba, wakati akizungumza na Nipashe.

Mtagwaba alisema wanahitaji kupata makandarasi wenye kuzingatia kazi yenye ubora na thamani ya pesa ya miradi yenyewe.

Meneja huyo alisema hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya makandarasi wavivu wanaotekeleza miradi nje ya makubaliano na kwamba wamejipanga kuhakikisha barabara zitakazofanyiwa kazi kwa mwaka 2020/21 zinawanufaisha wananchi wa maeneo husika kwa muda mrefu.

## 'Wanawake, vijana hawatafanikiwa bila kuungana'

**Na Halfani Chusi**

OFISA Uwezeshaji Kiuchumi Wananchi Manispaa ya Ilala, Asenga Georgisi, amewataka kinamama na vijana kujiunga katika umoja wa vikundi ili kujikwamua kiuchumi kupitia fursa zinazopatikana, ikwiamo mikopo.

Alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya uzinduzi wa Umoja wa Vikundi vya Ujasiriamali Kivule (Uvuki), akisisitiza kuwa kupitia umoja huo, itakuwa rahisi kuwawezesha kinamama kupata mikopo kiurahisi na kwa riba nafuu kwa kuwa vikundi hivyo vimesajiliwa kisheria.

"Huu ni mfano wa kuigwa, watu wanapozindua umoja wao itasaidia kupata mikopo na kurejesha bila migogoro kwa kuwa wanavikundi wote mnaamininiana na mnajuana. Hii pia itakuwa rahisi zaidi kuleta ushawishi kwa serikali katika kuwasaidia wanavikundi kutimiza malengo yao," alisema.

Ofisa huyo aliongeza kuwa, itaondoa matatizo ya wanavikundi kuvurugana na kushindwa kufikia malengo pamoja na wanavikundi kupata nafasi ya kupata elimu ya ujasiriamali.

"Vikundi vingi vimeshindwa kufikia malengo kwa sababu ya kukosa umoja kama huu, muda mwingine wanavikundi wanakosa elimu kwa sababu ya kukosa umoja kama huu. Kupitia umoja huu, itasaidia wanaumoja kuondokana na dhana ya kukaa kwa muda mrefu bila mafanikio," alisema.

Mwalimu wa Wanachama wa Uvuki, Ayubu Ezekieli, alisema kupitia elimu wanayotoa kwa wanachama, kuna faida nyingi wamezipata ikiwamo kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

"Tangu nianze kutoa elimu hii kwa wanachama, kuna mafanikio mengi ambayo tumeanza kuyapata ikiwamo baadhi yetu tumefanikiwa kujenga, kuwapeleka watoto shule, kupata mitaji na kutoa elimu ya kuwawezesha kujikwamua kiuchumi kinamama na vijana," alisema.

Mwalimu huyo aliwataka wanavikundi wengine kujiunga na umoja huo ili kufikia malengo yao kiurahisi na kwa njia rasmi.

Mwenyekiti wa umoja huo, Monika Benedict, alibainisha kuwa licha ya uwapo wa mafanikio makubwa kupitia umoja huo, wanakabiliwa na vikwazo kadhaa ikiwa ni pamoja na baadhi ya wanachama kutorejesha mikopo kwa wakati.

"Ni kweli kwamba umoja huu una mafanikio makubwa sana kwetu, lakini tuna changamoto kadhaa kwani baadhi ya wenzetu wamekuwa wagumu kurejesha mikopo kwa wakati, na wengine kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya suala zima la elimu ya ujasiriamali na ndiyo maana pia katika umoja huu tuna walimu ambao kazi yao ni kuendelea kutoa elimu juu ya ujasiriamali ili kadri siku zinavyozidi kwenda watu wabadilike," alisema.



# NMB yatoa misaada thamani ya mil. 11/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya NMB, imetoa msaada wa mashuka 180, kwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na madawati 50 kwa Shule ya Msingi Mnadani ya jijini Dodoma, ikiwa ni sehemu ya kurudisha faida kwa jamii.

Akizungumza katika hafla fupi ya kukabidhi misaada ya vitu mbalimbali yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 11, Meneja wa NMB kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema msaada huo ni sehemu ya faida walioipata.

Mlozi alisema katika kipindi cha mwaka huu, Mkoa wa Dodoma ndio unaoongoza kwa kupata misaada mingi kutoka benki hiyo. Alisema hadi sasa benki imeshatoa vitu vyenye thamani ya Sh. milioni 120.

Alisema kutokana jiji la Dodoma kuendelea kukua na kuongezeka idadi ya watu kila siku, mashuka hayo 180 yatasaidia kupunguza changamoto zilizo kwenye wodi mbalimbali katika hospitali hiyo.

"Hivi sasa jiji la Dodoma linakua kwa kasi sana na idadi ya watu inazidi kuongezeka, hivyo tumeona tuunge mkono juhudi za serikali katika kutoa msaada wa haya mashuka ambayo yatapelekwa katika wodi mbalimbali," alisema Mlozi.

Kuhusu msaada wa madawati, alisema yamegharimu zaidi ya Sh. milioni tano ikiwa ni ombi kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma.

"Madawati haya 50 tunayakabidhi leo ni maombi ya ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma kukabiliana na uhaba wa madawati katika shule zetu za msingi za mkoa wa Dodoma," alisema.

Pia benki hiyo ilikabidhi ndoo 50 za kunawia mikono ikiwa ni sehemu ya kuendeleza usafi ili kukabiliana na magonjwa mbalimbali ya mlipuko ikiwamo maambukizi ya virusi vya corona.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma (RMO), Dk Best Magoma, alisema wanaishukuru NMB kwa msaada huo.

Dk. Magoma alisema kuwa kitendo hicho kinaonyesha ni jinsi gani benki hiyo imekuwa karibu na jamii katika kusaidia sekta nyeti za afya na elimu nchini.

# Bodaboda wataka wachukuliwe hatua, si kunyang'anywa vyombo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MADEREVA wa pikipiki za abiria, maarufu kama bodaboda, wameiomba serikali kushughulikia kesi zitokanazo na makosa ya barabarani kwa mujibu wa sheria kuliko kuchukua vyombo vyao na kuviweka kwenye vituo vya polisi kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Bodaboda Mkoa wa Dar es Saalam, Mariam Msafiri, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akitoa mapendekezo kwa serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika kulinda kazi zenye staha kwenye sekta ya usafirishaji.

Msafiri alisema wizara kupitia Jeshi la Polisi inatakiwa kushughulikia kesi zinazohusu vijana walio kwenye sekta ya usafirishaji zitokanazo na makosa ya barabarani badala ya kukamata vyombo vyao vya usafiri.

"Jeshi la polisi linapaswa kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani ikiwamo kutoza faini zilizoainishwa kisheria kuliko kuchukua vyombo vyao vya usafirishaji na kuviweka kwenye vituo vya polisi kwa muda mrefu bila kesi husika kushughulikiwa," alisema.

**Elimu itasaidia kukuza uelewa na ujuzi wa matumizi sahihi ya barabara na vyombo hivyo ili kupunguza ajali zinazosababisha vifo, ulemavu na kuathiri jitihada za serikali kukuza uchumi na kuongeza kipato kwa vijana.**

Pia alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine, ipanue fursa za utoaji elimu ya mara kwa mara kwa vijana wanaojihusisha na usafiri wa bodaboda ikiwamo matumizi sahihi ya barabara na vyombo vyao vya usafiri.

"Elimu itasaidia kukuza uelewa na ujuzi wa matumizi sahihi ya barabara na vyombo hivyo ili kupunguza ajali zinazosababisha vifo, ulemavu na kuathiri jitihada za serikali kukuza uchumi na kuongeza kipato kwa vijana," alieleza Msafiri

Pia alisema Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hasa Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine, inapaswa kukuza ulinzi na kuboresha uhusiano wa kikazi ili kuongeza ufanisi katika sekta ya usafirishaji na usindikaji.

"Hii inatokana na kuwapo kwa uhusiano duni kati ya vijana walio kwenye sekta ya usafirishaji (bodaboda) na polisi," alisema.

Vile vile, alisema wizara hiyo kupitia vyombo vya ulinzi na usalama, isaidie kudhibiti matukio ya madereva wa bodaboda kuporwa vyombo vyao vya usafiri na hata wakati mwingine kuuawa.

"Vyombo vya dola vifanye uchunguzi wa haraka pale inapotokea dereva wa bodaboda ameporwa chombo chake au ameuawa akiwa kwenye shughuli yake ya usafirishaji," alisema.

Alisema pia serikali kupitia vyombo vyake kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) viendelee kukagua ubora wa vifaa kama vile kofia ngumu na vifungashio vya bidhaa zitokanazo kwenye sekta ya usindikaji.

Akizungumza katika kikao hicho kilichoandaliwa na shirika linajihusisha na masuala ya vijana la YPC, Mkurugenzi wa Kitengo cha Kushughulikia Malalamiko katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kamishna wa Polisi Albert Nyamhanga, alisema ameyapokea mapendekezo hayo kwa niaba ya serikali na yatafanyiwa kazi.

"Nimepokea mapendekezo haya kwa niaba ya serikali na nitayawasilisha sehemu sahihi, lakini niwahakikishie kuwa serikali inaendelea kutunga sera na sheria mbalimbali ambazo zitasaidia uwepo wa kazi zenye staha nchini"alisema Kamishna Nyamhanga.



Katibu wa wawakilishi wa vijana wanufaika wa mafunzo ya ufundi stadi yanayoratibiwa na mpango wa Taifa wa kukuza ujuzi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Vijana, Ajira na Wenye ulemavu, Godfrey Mbowe, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuipongeza serikali kutokana na ufadhili huo, Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wahitimu VETA wataka kutambuliwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imetakiwa kuwatambua vijana waliowezeshwa mafunzo mbalimbali katika vyuo vya ufundi ili iwatumie katika miradi mikubwa na ya kimkakati ambayo imekuwa ikitekelezwa nchini.

Katibu wa Vijana 59,684 waliofadhiliwa na serikali, Godfrey Mbowe, alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kwa niaba ya wanufaika.

Mafunzo hayo yanatolewa kupitia Mpango wa Taifa wa Kukuza Ujuzi unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu.

Mbowe pia aliiomba serikali kuhakikisha inawatambua na kuwatumia vijana hao, kwenye miradi mbalimbali iliyopo na itakayojitokeza, ili waongeze kipato na uzoefu.

Alisema mpango wa mafunzo waliyojifunza kwenye vyuo hivyo vya ufundi yamewasaidia vijana wengi kutokana na kupata mwanga na kutambua namna wanavyoweza kujiendeleza katika jamii inayowazunguka na kufikia ndoto zao.

Pia alisema vijana wengi wamejiajiri na kuajiriwa kupitia elimu waliyoipata kwenye mafunzo stadi na baadhi yao wameajiriwa kwenye taasisi, viwanda na sekta mbalimbali za uwekezaji kama vile ujenzi wa reli, barabara, vituo vya afya, maji na umeme.

Vijana hao pia wameiomba serikali kuhakikisha mafunzo yanayotolewa kwenye vyuo hivyo yanakuwa endelevu na kubuni miradi mingine ambayo inaendana na mahitaji ya hali ya uchumi kwa sasa ili kutengeneza ajira nyingi.

"Sisi vijana tulionufaika na mafunzo hayo ambayo yanadhaminiwa na serikali chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wengi wamejiajiri kupitia elimu waliyoipata ya mafunzo stadi. Baadhi yao wameajiriwa pia kwenye taasisi, viwanda na sekta mbalimbali za uwekezaji," alisema.

Mwenyekiti wa Vijana hao, Alfa Chitema, alisema kupitia mafunzo hayo wamepata hamasa kubwa kwa kuwawezesha kushirikiana na serikali ambayo hivi karibuni wameshuhudia ikiingia kwenye uchumi wa kati.

Alisema kabla ya kupata mafunzo hayo vijana wengi walikuwa wamekata tamaa na hawakuwa na kazi na wengine walijihusisha na uhalifu.



# Wanawake bado nyuma katika uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

LICHA ya dhamira ya serikali ya kufikia usawa wa kijinsia katika uongozi asilimia 50 kwa 50, wanawake bado wako nyuma katika nafasi za uongozi, imeelezwa.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Tanzania, Alhad Mussa Salum, alipokuwa akizungumza katika mkutano kuhusu nafasi ya mwanamke kuelekea uchaguzi mkuu, uliofanyika mjini hapa.

Salum ambaye pia ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema viongozi wa dini na wa kamati ya amani, wamekuwa wakihamasisha jamii kuona umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo kuhusu nafasi ya uongozi kwa mwanamke.

**Kwa mujibu wa Reuben, kwa sasa takwimu zinaonyesha wanawake walioko katika ngazi za uamuzi ni asilimia 37.**

Alisema ziko sababu nyingi zinazomkwamisha mwanamke katika nafasi ya uongozi na moja kati ya vikwazo vya mwanamke kupata uongozi ni mfumo dume ndani ya vyama vya siasa.

Salum alisema imebainika kwamba vyama vingi vya siasa vinawatumia wanawake katika shughuli za uhamasishaji katika kuongeza idadi ya wanachama na kueneza sera za chama ikiwamo wakati wa kampeni katika kuwavuta wapigakura.

"Kwa asilimia kubwa vyama vya siasa havimwoni mwanamke kama ni mdau kwa ajili ya nafasi ya uongozi na kushika nafasi ya uongozi na kushika nafasi ya nguvu ya kimaamuzi," alisema.

Pia alisema vikwazo vingine ni nguvu ndogo ya mwanamke kiuchumi, rushwa, lugha dhalilishi, mila potofu na kusababisha baadhi ya wanawake washindwe kujiamini katika kukabiliana na vitendo mbalimbali vya ukatili wa kijinsia.

Alisema kamati ya amani na viongozi wa dini inasisitiza umuhimu wa nafasi ya mwanamke katika uongozi juu ya nafasi mbalimbali kwa kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika kuinua uchumi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA) Rose Reuben, alisema ushiriki wa wanawake katika siasa na ngazi za uamuzi ni eneo lililo na changamoto nyingi, hivyo linahitaji kuhimizwa na viongozi wa ngazi za juu, asasi za kiraia, wanawake wenyewe na viongozi wa dini.

Kwa mujibu wa Reuben, kwa sasa takwimu zinaonyesha wanawake walioko katika ngazi za uamuzi ni asilimia 37.

Alisema mapengo hayo ni pamoja na lugha dhalilishi wakati wa uchaguzi zinazowakatisha tamaa wanawake kuwania nafasi za uongozi, uteuzi usiozingatia jinsia ndani ya vyama vya siasa, hofu na kutojiamini kwa baadhi ya wanawake wenye nia ya kugombea na ilani za vyama zisizozingatia jinsia.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib, alisema wanawake wanapopewa nafasi za uongozi huwa waaminifu na hufanya kazi kwa bidii.



Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, akitembelea eneo la mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani Chamanangwe Wilaya ya Wete Pemba na (kushoto kwa Rais) Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar Balozi Amina Salum Ali na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba Omar Khamis Othman. **PICHA: IKULU**

# Dk. Shein asifu maendeleo ya karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imefanya juhudi za makusudi katika kulibadilisha zao la karafuu kupitia Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ili liende na wakati uliopo.

Dk. Shein aliyasema hayo katika ufunguzi wa kiwanda cha kusarifu majani makavu huko Mgelema, Chake Chake, Kusini Pemba ambacho kimejengwa kwa ushirikiano wa ZSTC na Kampuni ya INDESSO kutoka Indonesia. Alisema hivi sasa ZSTC inakwenda kwa mabadiliko ya biashara na matumaini yake ni kwamba uongozi uongozi ujao utayaendeleza.

Serikali anayoiongoza, alisema iliongeza bei ya karafuu kutoka Sh. 3,500 hadi 14,000 kwa kilo huku ikisisitiza kuwa hata soko la dunia likishuka, serikali itaendelea kuwalipa wakulima kwa bei hiyo hiyo.

Aliongeza kuwa uwekezaji huo ni uhusiano na ushirikiano mwema kati ya Zanzibar na Indonesia.

Kwa mujibu wa Dk. Shein, serikali ya Zanzibar imeamua kujenga kiwanda hicho kwa kuwa Mgelema na Ngomeni ni nguzo kubwa ya uzalishaji wa zao la karafauu.

Rais Shein alisema katika kuhakikisha uimarishaji wa zao la karafuu pamoja na bidhaa zake, serikali imeamua kwa makusudi kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, kazi ambayo inatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Alisema tayari serikali imeshajenga barabara ya Ngomeni pamoja na kupeleka kituo cha afya, umeme na huduma zingine, hivyo baada ya miezi miwili barabara ya kutoka Kipapo hadi Mgelema itajengwa na kuahidi kuwa maisha ya wananchi wa kijiji hicho yatabadilika.

Pia alisema wananchi wa Zanzibar ndio waliopanda mikarafuu lakini wao hawakunufaika nayo badala yake walinufaika watawala waliotoka nje kuitawala Zanzibar.

Rais Dk. Shein alisema bado karafuu ya Zanzibar inatakiwa na inapendwa kwa kuwa bado soko lake lipo na tayari hivi sasa karafuu imerudi hadhi yake na hata magendo ya karafuu yamepungua.

Naye Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, alisema kiwanda hicho kitachangia kwa kiasi kikubwa kipato kwa wananchi hasa vijana ambao ndio wanaojishughulisha kwa kiasi kikubwa na shughuli za kiwanda hicho.

Akitoa taarifa za kitaalamu, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Juma Hassan Reli, alisema kiwanda kitakuwa na uwezo wa kusindika kilo 250 za majani makavu kwa wakati mmoja na kutoa lita saba za mafuta.

Alisema kitakuwa kikifanya kazi kwa muda wa masaa 24 na hivyo kuwezesha kupatikana lita 21 za mafuta kwa siku.

Balozi wa Indonesia nchini, Dk. Ratlan Pardede, alisema uzinduzi wa kiwanda hicho unaonyesha uhusiano mwema na ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na Indonesia.

# Katibu asisitiza vita dhidi ukatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Tawala Mkoa wa Kaskazini Unguja, Omar Hassan Masoud, amesema serikali itaendelea kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ili kupata taifa bora.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja katika uzinduzi wa Tamasha la Elimu bila Malipo lililofanyika katika Shule ya Nungwi Wilaya ya Kaskazini A', alisema ni vyema walimu na viongozi kushirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha vitendo hivyo katika jamii vinachukuliwa hatua zinazostahiki.

Kuhusu suala la elimu, aliwataka wanafunzi kufanya bidii katika masomo yao ili wapate maendeleo kwa ajili ya kuwa wajenzi imara katika taifa.

Alisema viongozi na waasisi waliopita wamefanya juhudi kubwa za kuimarisha suala la Elimu, hivyo ni vyema kufuata nyayo zao katika kuenzi elimu bila ya malipo na kuacha kuibeza.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk Idrissa Muslim Hija, alisema wizara itaendelea kushirikiana katika kuimarisha elimu kwa wanafunzi pamoja na kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi vinavyojitokeza katika jamii.

Mkurugenzi wa Michezo na Utamaduni wa Wizara hiyo, Hassan Khairallah Tawakal, alisema walimu hawana budi kuwa walinzi katika shughuli za elimu bila malipo zenye mnasaba wa kusherehekea na kufahamu historia ya mwaka 1964.



**TOMMY**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



## CHECHE LITAWACHOMA

# Diamond, Zuchu mahaba tele

SIKU chache zilizopita, Staa wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz na msanii wake katika lebo ya WCB, Zuchu, wametoa nyimbo mpya mbili ambazo zimeibua mjadala mkali.

Mashabiki wa wanamuziki hao, hawakuibua mjadala kutokana na nyimbo kali walizoimba, bali inatokana na maneno yenye hisia kali yaliyokuwemo katika nyimbo hizo mbili za Cheche na Liwatachoma.

Baadhi ya mashabiki ambao wamefuatilia akaunti za wanamuziki hao, walionekana kupagawa zaidi na utamu wa nyimbo hizo, lakini wasiwasi wao unatokana na maneno yenye hisia katika nyimbo hizo zinaweza kuleta jambo kwa wanamuziki hao.

Wakitoa maoni yao, baadhi yao walisema maneno yaliyomo kwenye nyimbo hizo, yanaweza kuwa na maana kubwa kati ya Diamond na Zuchu.

Hata hivyo, wasiwasi huo ulionekana kumkera mama yake Zuchu, Khadija Kopa, baada ya kuwajibu watu wanaotilia shaka nyimbo hizo kwamba wanapoteza muda.

Katika ujumbe wake kwa mwanawe, Kopa alimtaka binti yake kufumba macho kwani kwenye mafanikio atapata maneno ya kumkatisha tamaa, hivyo atazame mbele.

Kwa ujumla katika nyimbo hizo, Diamond na Zuchu wamezitendea haki baada ya kuimba kwa umahiri mkubwa na kuonyesha vipaji vyao halisi.

**BASI SAWA**

## Maria atambulisha ‘Fursa’ kwa wote

MSANII chipukizi wa Bongo Fleva, Mary Willium, maarufu kama Maria, ametambulisha singo yake mpya inayoitwa ‘Fursa’ ambayo imeanza kusikika katika vituo mbalimbali vya redio na Televisheni.

Akizungumza na BT, Maria, amesema wimbo wake huo utaleta mapinduzi hasa kwa waimbaji wa kike kutokana na aina ya muziki wake kuwa tofauti.

Amesema ameamua kuimba ‘Fursa’ kwa lengo la kuweka changamoto kwa waajiri binafsi na serikali kutoa nafasi kwa wanyonge kuonyesha vipaji vyao katika kazi.



“Nimeamua kuchagiza kwa kutumia wimbo ili kutoa sauti kila mtu ana uwezo wa kuonyesha kipaji chake kama akipatiwa fursa, jambo la muhimu watoaji wa nafasi lazima wawaamini na kuwasaidia,” amesema Maria.


Kuhusu kipaji chake cha uimbaji, amesema amekirithi kutoka kwa baba yake mzazi ambaye alikuwa mpigaji wa ala za muziki pamoja na

## Petitman ungenuna, yote usingeyapata

MENEJA na mjasiriamali, Metitman, amejitokeza na kueleza alikuwa akipata shida baada ya watu kumuona kama mbeba pochi wa mwigizaji nyota Wema Sepetu.

Akizungumza katika kipindi cha Planet Bongo cha East Africa Radio, meneja huyo Petitman, amesema licha ya kuitwa jina hilo, hakuweza kukata tamaa kwa kuwa yeye na Wema wametoka mbali na asingemuacha njiani.

“Zamani nikitukanwa mitandaoni ilikuwa inaniuma sana hadi nachanganyikiwa siku nzima, kuanzia kuitwa mbeba pochi wa Madam Wema Sepetu, lakini sasa hivi hata siumii kwa sababu hakuna tusi jipya” amesema Petitman Wakuache .





## Tommy Favour kumbe unajua kupenda

MSAMNII wa BongoFleva, kutoka lebo ya Kings Music, Tommy Flavour, amesema mvutano wa kimapenzi kati yake na Official Lyyn, ulianzia ndani ya chumba cha kurekodia muziki.

Akizungumzia uhusiano huo, kwenye kipindi cha Planet Bongo, Tommy Flavour, amesema kuanzia siku hiyo mapenzi yamezidi kuchanua kutokana na yeye kuwa mkweli siku zote.

“Kitu ambacho nimefanya hadi kuweza kutulia na Official Lyyn ni misingi ya kuwa mkweli, kingine labda kuna vitu tofauti ameviona kutoka kwangu ndiyo maana nimetulia naye, nakumbuka tulikutana studio na tukaanza urafiki ila urafiki wetu ukazidi, uhusiano yetu yana muda wa miezi saba tangu tuwe pamoja” amesema Tommy Flavou.



## Bonge La Nyau asimulia alivyonusurika

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Bonge la Nyau, ambaye anauguza majeraha baada ya kupata ajali mbaya ya gari, amesema anachokumbuka siku ya tukio ni mwanga mkali na kelele za Lulu Diva za kuomba msaada.

Akizungumza na EATV, Bonge la Nyau, amesema mwanga huo ulitokana na lori kubwa kutokea ghafla mbele yao, ndipo dereva wao alipoamua kulitupa gari kwenye makorongo ili wasigongane uso kwa uso.

“Lori na lori zilikuwa zinashindana ku-overtake kisha lori moja likaingia kwenye njia yetu, ghafla tukaona mwanga mkali sana kwenye gari letu, mara nikaanza kusikia kelele za Lulu Diva akisema “mama nakufa, mama nakufa”, dereva wetu alikuwa kwenye mwendo na ilikuwa usiku hivyo akalitupa gari kwenye korongo ili mradi tusigongane uso kwa uso maana ndiyo ingekuwa mbaya zaidi” amesema.

## WAKIIMBA UTAUMIA KWA KUSIKITIKA

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEZI Mungu ametoa karama tofauti kwa binadamu. Wapo wenye vipaji vya michezo, kuigiza na hata kuimba.

Katika muziki kuna watu wamejaaliwa na vipaji vyao, kuna wapiga ala na kuimba pia.

Pia kwenye uimbaji kila mmoja amempa kipaji cha aina yake ya uimbaji. Wengine amewapa karama ya kuimba sauti za juu, wapo wa sauti za kati na za chini.

Hata staili za kuimba nazo watu wametofautiana. Kuna wanaoimba vizuri tu, lakini wapo wanaimba kwa sauti za huzuni na masikitiko.

Kwa upande Tanzania, ukiachana na Wilson Peter na George Peter ‘Kinyonga’, ambao wao wanaimba staili ya Mwambe lakini maisha yao yalikuwa nchini Kenya, wakiwa na Simba Wanyika, wapo ambao waliopiga muziki Tanzania na wakawa wanaimba kwa staili ya Mwambe.

**Mbaraka Mwinshehe**

Mbaraka Mwinshehe Mwaruka ni mmoja wa wanamuziki ambao ni nembo na alama ya muziki wa Tanzania.

Nadhani wengi wasichokijua ni aina yake ya uimbaji. Huyu ni mmoja wa waimbaji waliokuwa wakitumia staili ya Mwambe. Ukisikiliza nyimbo zake nyingi utagundua kuwa ana aina fulani ya uimbaji wa kulalamika na masikitiko na huzuni juu.

**TX Moshi William**

Nchini Tanzania, mashabiki wengi wa muziki wanamjua Tx Moshi William kuwa ndiye mwimbaji ambaye moja kwa moja alikuwa akiimba anaonekana kabisa kuwa analalamika.

Staili ya uimbaji wa Moshi, ilijipambanua kwa mashabiki wa muziki kuwa ni ya mwambe moja kwa moja na wala haina mjadala.

Wasichokijua wengi ni kwamba Moshi, aliiga staili ya uimbaji huo kutoka kwa George Peter wa Simba Wanyika. Lakini George alitamba zaidi Kenya na Moshi Tanzania.

Ukisikiliza nyimbo za Simba Wanyika, unaweza kugundua kuwa aina fulani ya uimbaji unaoshabihiana sana na uimbaji wa Moshi.

**George Mpupua**

Uingizaji wake kwenye muziki ulikuwa wa bahati tu, kutoka kwenye maktaba wa kutunza muziki na nyaraka za Redio Tanzania, hadi kuwa mwanamuziki mkubwa kwenye bendi za Mwenge Jazz, Uda Jazz, Vijana Jazz na nyinginezo.

Mpupua aliimba wimbo wa ‘Mwanahawa’ kwenye studio ya RTD, wakati Mwenge Jazz akirekodi. Awali ulikuwa vyombo vitupu, lakini yeye aliamua kuuwekea maneno. Kilichotokea ni kwamba ndiyo uliopendwa zaidi na mashabiki kuliko zote zilizorekodiwa na Mwenge Jazz siku hiyo.

Mwenge Jazz waliamua kufuata taratibu za kumuondoa maktaba RTD na kumfanya kuwa mwanamuziki. Aina yake ya uimbaji ni wa masikitiko na huzuni, huku akiwa na sauti nyembamba na nyororo.

**Mikidadi Seif**

Ukimsikiliza sana unaweza ukadhani Tx Moshi anaimba. Sikiliza nyimbo za ‘Nenda Kaishi Salama’, na ‘Tulele Tubhoe’.

Naye pia siku chache kabla hajafariki katikati ya mwaka huu, alihojiwa na kusema kuwa alimpenda sana George Peter wa Simba Wanyika. Hiyo tu ilitosha watu kujua kuwa ndiyo maana uimbaji wake ulifanana na Moshi William. Ni ule ule wa masikitiko, na huzuni Mwambe.

**Patrick Balisidya**

Huyu ni kiongozi wa bendi ya Afro 70, iliyowika kwenye miaka hiyo. Balisidya alijitofautisha na bendi nyingine nyingi kutokana na aina yake ya uimbaji, ambapo nyingi zilikuwa ni za huzuni na masikitiko.

Hata kama nyimbo zenyewe si za maudhui hayo, lakini bado aina ya uimbaji ilikuwa ni ya masikitiko.



TX Moshi William

## Siri ya Majini: Kulelewa kuna gharama

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo wa kiswahili unaosema ‘bure aghali’. Maana yake kitu chochote cha bure huwa kina gharama yake. Ukienda mbali zaidi kwenye ufafanuzi ni kwamba chochote kinachoonekana kuwa hakina gharama, huwa kina kasoro, hivyo unaweza kukigharamikia mara kwa mara na kupoteza fedha nyingi, wakati kumbe ungeweza kukinunua kwa gharama kubwa mara moja tu.

Siku hizi kuna wimbi la vijana wanaopenda sana dezo, haswa kutoka kwa kinamama.

Vijana wengi hawataki kufanya kazi, hawajitumi, badala yake wanataka kuwamiliki wa-



nawake wenye pesa na mali.

Wakifanya masihara inaweza kuwatoka kama huyu wa kwenye filamu ya ‘Siri ya Majini’. Ni filamu nzuri, yenye mafundisho kwa jamii. Imechezwa na baadhi ya wasanii ambao ni Leah Mussa, Denis Luis, Warda Uwesu, Asha Jumbe, Juma Twalib, Debora Dickson na wengineo.

Ram ana mpenzi wake anaitwa Jacky. Lakini wakati Jacky akiwa safarini Ram anaanzisha mapenzi na msichana mwingine aitwaye Shamim.

Awali ilionekana ni mapenzi ya kawaida tu. Lakini Shamim alinogewa na kumtaka wafunge ndoa awe mkewe. Kutokana na Shamim kuonekana ni msichana mrembo na mwenye uwezo wa kipesa, Ram anakubali.

Hata hivyo, Ram baadaye alikuja kugundua kuwa Shamim hakuwa mke wa kawaida, bali alikuwa jini.

Kujiondoa kwenye mikono ya Shamim haikuwezekana tena, kwani tayari alionekana ameshajua siri hiyo, na Ram alipigwa mkwara wa nguvu kuwa akiondoka kwake, atafayiwa kitu kibaya.

Jacky aliporejea, aliungana na rafiki yake Ram alitwaye Jisu kumsaka na pamoja na kugundua anapoishi, lakini walifukuzwa kama mbwa.

Mapenzi ya binadamu na jini yalifanikisha kuzaliwa mtoto wa kike, lakini akifundishwa tabia zote za kijini na mama yake.

Katika kujiondoa kwenye minyororo ya jini Shamim, Ram anaamua kutafuta mganga ili kumdhuru Shamim, ili arejee nyumbani na kuungana na mpenzi wake aliyempenda kwa dhati, Jacky.

Zoezi linafanikiwa, lakini nusu. Shamim anaungua mwili mzima, na akatambua kuwa zile zote ni njama za mume wake Ram.

Jambo hili linamkasirisha mno jini Shamim. Anamwambia wazi kuwa si jambo la kawaida jini kumlilia au kumpenda binadamu, lakini yeye amefanya hivyo kwa sababu amempenda sana, lakini matokeo yake anakuja kumfanyia mambo kama yale.

Mwisho wa siku, Shamim anaamua kumuua Ram, lakini na yeye anashtukia anauawa. Taarifa hizi zikaletwa kwa Jisu na binti wa Ram aliyezaa na jini Shamim, anaitwa Muna.

Muna, ambaye ana umbile la kibinadamu, lakini mwenye uwezo wa kijini, alimwambia baba yake mdogo Jisu kuwa yeye hawezi kuishi pale, anakwenda kuishi na majini wenzake, ila atakuwa anakuja kuwatembelea.



# Idris Elba atarajia kupata mtoto

MWIGIZAJI kutoka Uingereza, Idris Elba na mke wake Sabrina Dhowre , wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Staa huyo alitwiti hivi karibuni akimshukuru mke wake huyo kwa kutarajia kumpatia mtoto wake wa kwanza.

"Sabrina nakushukuru kwa yote, nakupongeza kwa kuniletea mtoto, siwezi amini kwa yote unayonifanyia, kaa salama," ameandika Elba.



## Chike lisemwalo lipo

STAA wa filamu kutoka Nollywood,Chike Ike, hatimaye amekanusha uvumi kwamba anatoka kimapenzi na mume wa rafiki yake, Regina Daniel.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Chike, amesema hana uhusiano na mwanaume huyo,Ned Nwoko, ambaye ni tajiri wa kupindukia na kinachoenezwa mitandaoni hakina ukweli.

"Hapana, sina na sina wazo la kuwa na mtu mwenye wake saba, hilo haliwezekani kamwe," amesema Chike.

## BBNaij washiriki waanza kupata neema

WASHIRIKI wa shindano la maisha halisi la Big Brother Nigeria, limeingia katika hatua muhimu baada ya watatu kushinda nafasi ya ubalozi wa urembo.

Katika kuwatafuta mabalozi hao, washiriki wakiwa katika makundi ya watu watatu, walishindana kuelezea urembo wa Kiafrika ikiwamo utunzaji wa nywele.

Shindano hilo ambalo liliendeshwa na kampuni ya Darling, kundi linaloundwa na Nengi, Prince na Trikkytee liliibuka na ushindi wa jumla.





## Mwigizaji msomi Nigeria afariki dunia

SEKTA ya filamu nchini Nigeria, imekumbwa na simanzi baada ya mkongwe katika sanaa hiyo, Prof. Ayobami Akinwale, kufariki dunia.

Kabla ya kifo chake, Prof. Akinwale, alikuwa akifanya kazi katika idara ya sanaa ya jukwaani katika Chuo Kikuu cha Ilorin.

Akinwale alianza kujulikana kwenye uigizaji mwaka 1997, baada ya kutoa filamu ya Sango, Ladepo Omo Adanwo (2005), Iranse Aje (2007), na zingine nyingi.

## Diana kweli umevunja amri ya Mungu?

MWIMBAJI maarufu wa Injili wa Ghana, Diana Asamoah, amesema ni jambo la aibu kwake kupata ujauzito kabla hajafunga ndoa.

Kulingana na kauli yake, Diana amesema hatatokea kupata ujauzito kabla ya kuolewa, kwani kufanya hivyo ni sawa na kumkosea Mungu.

Kauli hiyo ameitoa baada ya watu kusambaza picha katika mitandao ya kijamii wakisema msanii huyo ni mjamzito wa miezi kadhaa.



MAKALA



Wapigakura wakichagua viongozi katika maeneo mbalimbali. **PICHA: MTANDAO**

# Sehemu ya mwanahabari kipindi hiki cha uchaguzi

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI kampeni za uchaguzi zikiendelea kwenye majukwaa mbalimbali mijini na vijijini, jicho la wanahabari liko kazini, ili kuuhabarisha umma michakato inavyoendelea, wakitumia runinga, magazeti, mitandaoni na ndani ya redio.

Hiki ndicho kipindi wamiliki, wanahabari na viongozi wa vyumba vya habari kuanzia wakurugenzi, wahariri na wahiriri watendaji wanapohusika moja kwa moja na kudumisha na kuendeleza demokrasia.

Ni wakati wa kuhusika na kushiriki moja kwa moja kutoa na kusambaza habari pasipo woga au upendeleo lakini, kwa kuzingatia maadili, sheria, kanuni na taratibu za nchi na zile zinazolinda mchakato huo, na za kitaaluma ili kuheshimu haki za binadamu.

Wanahabari ndiyo wahusika wakuu wa kutoa elimu ya uchaguzi kwa umma kuwahabarisha umuhimu na malengo ya uchaguzi, kwanini kujiandikisha? Kutoa taarifa za ilani za uchaguzi na pia kuwatambulisha wagombea, kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria na vyombo vinavyousimamia uchaguzi.

Si jukumu la wanahabari kumsaidia mgombea kumtusi mwenzake kwenye majukwaa kwa kueleza taarifa za maisha yake binafsi kuanzia uhusiano wa ndoa, kufilisika, madeni na tabia zake pengine akidaiwa ni jambazi au muuaji.

Kama ambavyo inaaminika kuwa kura ni turufu ya kupata uongozi bora na maendeleo ndiyo ambavyo wagombea wanatakiwa kuzungumzia jinsi watakavyosaidia kuleta maendeleo siyo kuwafananisha wapinzani wao na vinyago au hawani.

Wanahabari hawaendi majukwaani kueneza siasa za majitaka za kuelezea ubaya wa mwanasiasa Fulani ni kwa sababu wagombea wanajinadi jinsi watakavyoleta maendeleo, hiyo ndiyo iwe ajenda si kudhalilishana.

Kwa sababu kura ni haki ya msingi ya kikatiba, kushiriki katika kuchagua viongozi watakaotumikia umma ni wajibu na siyo tu kupiga kura bali kuangalia mwenye sifa asiyehonga wapigakura au asiyewashurutisha kwa rushwa au kuwanunua ili wamchague.

Kama ambavyo wapigakura wako huru ndivyo navyo wanahabari walivyohuru katika kuripoti habari za uchaguzi.

Ni wazi kuwa kama ambavyo kura moja inaweza kuleta mabadiliko katika uchaguzi vivyo hivyo habari zinazochapishwa kwenye vyombo vya habari zinavyoweza kuleta mabadiliko kwenye kampeni.

Mabadiliko hayo yanaweza kuwa ya kumharibia mgombea, kumdhalilisha, kumshushia hadhi na kumsababishia wapigakura kumkimbia ua kumuona hafai.

Kama vile ambavyo wananachi wanaamini kuwa kura ina thamani kubwa, wapigakura wakihimizwa kujiandikisha , kufuatilia kampeni vivyo hivyo wanahabari nao wanalazimika kutumia kalamu , kamera na sauti zao ipasavyo kuripoti habari za wagombea na siyo kufanyakazi zinazoweza kuwachonganisha wagombea na wapigakura. Wajibu wa wanahabari ni kuheshimu na kulinda utu wa watu wakiwamo wagombea na mpigakura.

**Inabidi tuchague wa kutuwakilisha. Huyo ndiye mbunge. Ndiyo maana ya kupiga kura. Leo Oktoba 28, 2020. Je, tunafahamu kuwa hatuwezi kwenda wote kuzungumzia mambo yetu bungeni Dodoma ndiyo maana tunamchagua huyu kutuwakilisha?**

Kutangaza habari za mgombea fulani kwa kigezo cha kutaka kupatiwa 'kitu kidogo au rushwa' kunaweza kufananishwa na kuidhalilisha taaluma na utu wao kwa vile mlungula umepewa thamani kuliko mpigakura na hata mgombea.

Jamii ifahamu kuwa ni jukumu la wanahabari kuwahimiza wapigakura kuachana na kujidhalilisha na kuupuuza utu wao kwa kujithamanisha na dera, sukari, pilau , khanga, soda, bia au fedha.

Ni vyema wakawasikia wanapowaeleza kuwa ni haki na vyema kutumia haki yako ya kupiga kura na kumchagua wanayempenda badala ya kupeleka kura kwa kumchagua aliyekupa sukari na kanga. Ni vyema kukumbuka kuchagua kiongozi bora na si kuwaza soda au bia ulizokunywa.

Thamani ya kura ni kubwa siyo pesa, wali au vilemba wanavyopewa kinamama . Wananchi wanapopiga kura wanatakiwa kujifahamu na kujiambia kuwa " sisi wakazi wa jimbo kwa mfano la Kinondoni au Same Mashariki, Katavi, Chalinze au Arusha Mjini hatuwezi kwenda wote bungeni Dodoma kuzungumza masuala yetu."



"Inabidi tuchague wa kutuwakilisha.Huyo ndiye mbunge. Ndiyo maana ya kupiga kura. Leo Oktoba 28, 2020. Je, tunafahamu kuwa hatuwezi kwenda wote kuzungumzia mambo yetu bungeni Dodoma ndiyo maana tunamchagua huyu kutuwakilisha? "

Kama tunalifahamu hilo tunataka aweje? Kwa sababu tunatafuta wa kutusemea kwanini atuhonge? Ni kwa sababu gani anunue vitambulisho vya wapigakura wenzetu?."

Ndiyo maana wanahabari wanawahimiza wapigakura kufahamu kuwa thamani yao ni kubwa isiyoweza kupimwa au kulinganishwa na mgawo wa sukari, vitenge au madera. Kwa sababu hiyo wanawaelimisha umuhimu wa kupiga na kikubwa ni kufahamu kuwa ni ili kujipatia maendeleo. Lengo la uchaguzi ni kupata uongozi wa kuwaletea maendeleo.

Lakini, vile vile wagombea na wapigakura waelewe kuwa kazi ya mwanahabari wakati wa huu wa kampeni ni kutoa fursa sawa kwa wagombea kwa kuzingatia, washiriki wenye mahitaji maalumu, wanawake na wanaume pia

Kwa hiyo wasitegemee kuwa kazi ya waandishi na vyombo vya habari ni kupamba au kuchafua mgombea au chama ama kushawishi au kupotosha wapiga kura bali kutumia taaluma yao kudumisha demokrasia, umoja na kuleta maendeleo ya taifa kwa kuweka uzalendo na maslahi ya taifa mbele na si masuala binafsi.

Vyombo vya habari kwa upande mwingine vinahusika na kutoa ufafanuzi kwa masuala ambayo yanaleta sintofahamu. Ndiyo maana wananchi nao wafuatilie vipindi, habari na taarifa zinazoelimisha kuhusu uchaguzi ili kupata uelewa na ufafanuzi wa kutosha.

Kwa mfano umbali wa kukaa baada ya watu kupiga kura.

Pamoja na wajibu wa wanahabari Watanzania kuanzia vyama, wagombea , wadau na wapigakura nao wanawajibika kufanikisha kuwapo uchaguzi huru, wa haki na wa amani kwa kufuata sheria.


Mambo ya muhimu ni kuzitafuta na kuzijua sheria zikiwamo za kuzuia na kupambana na rushwa na kufuatilia Sheria ya Uchaguzi.

Pamoja na kufuatilia na kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni ni vyema pia kuzingatia mambo muhimu kama muda wa kuanza na kumaliza kampeni.

Mambo ya kufanya siku ya kupiga kura, sheria inasemaji kuhusu mavazi, kampeni ni nini maelekezo ya kisheria baada ya kupigakura.

# KUNA UHAI VENUS?

## • Mawingu yake yana gesi, vimelea • Wanasayansi wapata matumaini



Gesi aina ya  Phosphane PH3, ni molekyuli inayoundwa kutokana na atomu moja ya Phosphorous na tatu za Hydrogen.

**Na Mwandishi Wetu**

UGUNDUZI mpya umeanza kuleta matumaini kwamba siku moja watu wataanza kuishi katika sayari nyingine tofauti na Dunia.

Wazo hilo linazidi kuleta ushawishi baada ya hivi karibuni wanasayansi kugundua kuna dalili ya kuwa na uhai katika sayari ya Venus au Zuhura.

Katika utafiti huo, wameonekana viumbe wanaoishi wakielea katika mawingu ya sayari hiyo.


Wanasayansi hao wakitumia darubini yenye nguvu kuchunguza anga za juu, wamegundua gesi inayojulikana kwa jina Phosphane PH3, ambayo ni molekyuli inayoundwa na atomu moja ya Phosphorous na tatu za Hydrogen.

Phosphine, ni sumu ambayo una harufu mbaya inayoundwa na wadudu wadogo wenye uhai.

Kwenye ugunduzi huo, jambo la kufurahisha na linachochea kufanyika kwa uchunguzi wa kina ni kujua ishara ya uhai katika sayari hiyo inatokana na nini.

Phosphane inapatikana katika viumbe vidogo wanaoishi katika koo za wanyama kama vile Pingu au sehemu zenye mazingira mabaya ya hewa kama vile kwenye madimbwi vya maji chini ya ardhi.

**Tangu niaze kazi yangu nimekuwa na hamu kujua iwapo kuna uhai katika maeneo mengine ya ulimwengu, hivyo nafurahi kwamba hilo linawezekana.**



Mwonekano wa sayari ya Venus

Pia gesi hiyo inaweza kuzalishwa viwandani kwa kutumia kemikali maalum.

### INAPATIKANA KILOMITA 50

Katika jambo linaloshangaza gesi hiyo imeonekana umbali wa kilomita 50 kwenye mawingi kutoka ardhini.

Profesa Jane Greaves, kutoka chuo kikuu cha Cardiff na wenzake, wanajiuliza swali kama hilo, lakini bado hawajapata jibu sahihi.

Katika taarifa yao waliyochapisha katika jarida la asili ya anga, inaeleza ugunduzi wao huo wa Phosphine katika sayari ya Venus, inaonyesha molekyuli hiyo inaweza kuwa na chanzo asilia na kisicho cha kibaiolojia. Lakini kwa sasa hata wao wamebaki njia panda.

Hata hivyo, hakuna aliyefanikiwa kuelezea chanzo cha Phosphine iliyogunduliwa kibaiolojia. Kutokana na mkanganyiko huo, ina maana tosha kuwa kuna ishara za uhai katika sayari hiyo.

"Tangu niaze kazi yangu nimekuwa na hamu kujua iwapo kuna uhai katika maeneo mengine ya ulimwengu, hivyo nafurahi kwamba hilo linawezekana" , anasema Profesa Greaves.

Prof. Greaves, anatoa shinikizo kwa watu wengine kwenda mbali zaidi kitafiti ili kuona kama kuna makosa wameyafanya.

"Nyaraka zetu na data ziko wazi, hivyo ndivyo jinsi sayansi inavyofanya kazi," anaongeza kusema.

### MAMBO YA KUSHANGAZA

Venus haipo katika orodha ya uwezekano wa kupatikana kwa uhai katika mfumo wa sayari inayozunguka jua, ukilinganisha na Dunia.

Asilimia 96 ya anga yake ina gesi ya kaboni. Kiwango cha joto katika sakafu yake ni zaidi ya nyuzi joto 400.

Vifaa vya angani vilivyotua katika sayari hiyo, vimechukua dakika chache kabla ya kuharibika kutokana na joto kali.

Hatahivyo umbali wa kilomita 50 kaskazini viwango vya joto sio vya juu.

Eneo hilo ndiko kunaaminika kuna dalili ya uhai katika sayari ya Venus.

### MAWINGU MAZITO

Hofu inakuwa kubwa kuishi katika sayari ya Venus, kutokana na mawingu yake kuwa mazito na yenye tindikali.

Mawingu hayo yana asilimia 75 hadi 95 za tindikali aina ya Sulphuric, ambayo ni hatari kwa viumbe vinavyoishi duniani.

### WENGINE WANASEMAJE?

Hata hivyo, kuna wasiwasi mwingi katika ugunduzi huo kutokana na wataalamu hao waliofanya utafiti kutokuwa na uhakika wa kupata uhai katika sayari ya Venus.

Badala yake  jopo hilo linasema wazo linahitaji kuchunguzwa zaidi kutokana njia za kibaiolojia au kutumia kemikali ili kuthibitika.

Njia pekee inayoweza kutumika ni kutuma kifaa maalumn kwenda kufanya uchunguzi katika anga ya sayari ya Venus. NASA hivi majuzi iliwauliza wanasayansi kama wanaweza kutuma ujumbe utakaokwenda kwenye sayari hiyo mwaka 2030.

Roboti zinapendekezwa kusafiri kupitia mawingu ya Venus.

## HABARI KIMATAIFA



Ndege maalumu ikizima moto karibu na eneo la Juniper Hills, California nchini Marekani jana. **PICHA: REUTER**

# China na Marekani zaonyeshana ubabe

**BEIJING,** China

CHINA imesema inafanya mazoezi ya kijeshi karibu na mlango wa bahari wa Taiwan, wakati maofisa wa Marekani wakitembelea kisiwa hicho.

Mazoezi hayo ya kijeshi yanafanyika wakati kukiwa na mvutano kati ya Marekani na China kuhusu hatma ya kisiwa hicho. Wakati Marekani ikiahidi kutoa msaada wake, China inaichukulia Taiwan kama jimbo lililojitenga.

Mjumbe wa juu kutoka Wizara ya mambo ya Nje ya Marekani, alifanya ziara kwenye kisiwa hicho mara kadhaa. Jana msemaji wa Wizara ya Ulinzi nchini China, Ren Guoqiang, aliishutu ameishutumu Marekani na Taiwan kwa 'ushirika wao wenye hila na kusababisha migongano.

**Mazoezi ya kijeshi yalikuwa halali na muhimu kwa eneo la bara kwa ajili ya kulinda himaya na uaminifu.**

Aliwaambia waandishi wa habari huku akiepuka kuzungumzia ziara hiyo, alisema 'kuitumia Taiwan kuidhibiti China au kutegemea nchi za kigeni kujiimarisha ni mawazo ya kufikirika.

"Mazoezi ya kijeshi yalikuwa halali na muhimu kwa eneo la bara kwa ajili ya kulinda himaya na uaminifu," alisema.

Krach, ambaye ni ofisa chini ya Waziri wa Marekani anayeshughulikia masuala ya uchumi, jana alikutana na Rais wa Taiwan, Tsai Ing-wen.

Marekani haina uhusiano wa kibalozi na Taiwan, hata hivyo, sheria ya mwaka 1978 inaruhusu kuuza silaha na kufanya urafiki wa karibu. **BBC**

## Wanajeshi wa Uturuki wauawa

**ANKARA,** Uturuki

WIZARA ya Ulinzi ya Uturuki, imesema Wanajeshi wake wawili wameuawa na mmoja amejeruhiwa baada ya wapiganaji wa Kikurdi kurusha makombora katika kambi ya kijeshi kaskazini mwa Iraq.

Nchi hiyo inapigana na wapiganaji wa chama cha Wafanyakazi wa Kikurdi (PKK), katika maeneo ya Kusini mashariki na Kaskazini mwa Iraq.

Mwezi Juni mwaka huu, ilianzisha mashambulizi mapya ya ardhini yaliopewa jina la "Operation Claw-Tiger" ambapo wanajeshi wa Uturuki waliingia zaidi ndani ya Iraq.

Katika taarifa tofauti, Wizara ya mambo ya ndani ya Uturuki ilisema wapiganaji 71 wa PKK wameuawa na wengine 38 wamekamatwa tangu kuanza kwa opresheni hiyo. **DW**

**Mwezi Juni mwaka huu, ilianzisha mashambulizi mapya ya ardhini yaliopewa jina la "Operation Claw-Tiger" ambapo wanajeshi wa Uturuki waliingia zaidi ndani ya Iraq.**

## Watu milioni 300 hatarini kwa njaa

**NEWYORK,** Marekani

SHIRIKA la mpango wa chakula duniani (WFP), limeonya watu milioni 300 wanakabiliwa tishio la na baa la njaa kutokana na mizozo, mabadiliko ya tabia nchi na janga la Covid-19.

Mkuu wa shirika hilo, David Beasley. Alitoa wito huo kwa wahisani ili kusaidia kukabiliana na hali hiyo.

Beasley aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa onyo alilolitoa miezi mitano iliyopita na kufanyiwa kazi, imesaidia kuzuia janga la njaa.

Alisema WFP na washirika wake wamejaribu kuwafikia watu milioni 138 mwaka huu, idadi hiyo ni kiwango kikubwa cha watu kusaidiwa katika historia na shirika hilo.

Hata hivyo, alionya kuwa watu milioni 270 wanakabiliwa na njaa. Tayari watu milioni 30 wanategemea chakula kutoka WFP na huenda wakafariki iwapo watakosa msaada huo.

Mataifa ambayo yanakabiliwa na njaa ni Congo, Yemen, Sudan Kusini na Nigeria. **DW**

## Mpaka wa Belarus, Poland upo wazi

**Warsaw,** Poland

WANAJESHI wanaolinda mpaka kati ya Belarus na Poland umesalia kuwa wazi, licha ya Rais Alexander Lukashenko kutangaza nchi yake itafunga mipaka yake.

Kiongozi huyo alisema mipaka itakayofungwa ni ile ya nchi za Poland na Lithuania. Ofisa mmoja wa Poland alisema mpaka huo uko wazi na hakuna ishara kuwa utafungwa.

Lukashenko anakabiliwa na shinikizo la kujiuzulu na raia wake wa Belarus, baada ya wiki kadhaa za maandamano. Belarus imetumbukia katika mzozo wa kisiasa kufuatia uchaguzi mkuu uliofanyika Agosti 9, mwaka huu, uliogubikwa na madai ya wizi wa kura. **DW**

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALUMU IDD KITULIKE** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 800 CZX** aina yake **NOAH** yenye ingine namba **35568976** na chasis namba **SR 400171061** na RB namba **MOR/MOR/RB/299851/2020.**

115906702

---

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
DISTRICT REGISTRY
AT DAR ES SALAAM

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 43 OF 2020**
In The Matter of the Estate of The Late Eunice Wambui Njenga
And
In The Matter of Application for Re-Sealing of Letters of Administration
By Bernard Njogu Njenga And Loise Njeri Njenga

**NOTICE OF APPLICATION FOR RESEALING**
***(Made Under Rule 99 of Probate Rules GN No. 10/1963)***

Notice is hereby given that an application has been made to this Court for sealing of the Letters of Administration of the estate of **Eunice Wambui Njenga,** late of Nairobi province deceased, who died at **COPTIC Hospital** on the 17th day of July 2017, granted to **Bernard Njogu Njenga and Loise Njeri Njenga** of Nairobi by The High Court of Tanzania, At Dar es salaam and that the said application will be heard at this Court by a Judge in chambers on the 09th day of October 2020 at 10.00 o'clock in the forenoon.

Dated at **DAR ES SALAAM this 14TH day of SEPTEMBER** 2020.

REGISTRAR
Deputy Registrar
High Court of Tanzania
Dar-es-Salaam Zone

Presented for filling this 18th day of September 2020

DRAWN AND FILED BY
Gerald Mosha Jr. Esquire,
Office Accommodation Scheme Building
4th Floor, Azikiwe Street
P.O.Box 68
+255 715 111 589
DAR ES SALAAM

215907302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;278/2020**

**Ombi la (1) NAOMI P.NDAKI (2)MUSSA J.MLINGWA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JOSEPH JEREMIA MLINGWA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/09/2020.

Tarehe 16/9/2020
Sahihi ya Hakimu

115907202

---

**YONO AUCTION MART & CO. LIMITED**
**(DALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA)**
**P. O. BOX 693 DODOMA – BRANCH**
**MOBILE: 0754497124/ 0712514136/ 0785786470.**

**KUMB: NO. YONO/DOM/2020/08 14/09/2020.**

**UTEKELEZAJI WA AMRI YA BARAZA LA ARDI NA NYUMBA- DODOMA**

**SHAURI LA MADAI NO. 64/2020**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF NOOR MASJID DODOMA- MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF BARAZA KUU LA WAISLAMU TANZANIA(BAKWATA-DODOMA)**
**KWENDA: KWA THE REGISTERED TRUSTEED TRUSTEES OF BARAZA KUU LA WAISLAMU TZ(BAKWATA)**
**Husika na kicwa tajwa hapo juu**

Tambua kuwa hii ni AMRI YA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA. Ya kukuondoa kwenye nyumba tajwa hapo juu, kuwepo au kutokuwepo kwenye nyumba hiyo kutategemeana na hukumu ya shauri tajwa hapo juu itakapo malizika.

Hivyo basi mimi **DALALI WA MAHAKAMA** nitakuwa katika utekelezaji wa shauri hapo juu na kwa vile tupo katika utekelezaji wa amri ya mahakama unatakiwa uwe umehama/ mmehama kwenye nyumba hiyo ndani ya siku 14 ili dalali aweze kuendelea na utekelezaji, HIVYO BASI MPAKA TAREHE 29/09/2020 SIKU YA JUMANNE WOTE MUWE MMEHAMA/ KUONDOKA BILA KUKOSA, Mbali na hapo ukishindwa kuondoka/ kuhama, utekelezaji wa amri ya Mahakama utaendelea bila kupewa notisi nyingine tena.
KUMBUKA, Kushindwa kutii amri hii kutapelekea hatua kali za kisheria kuchukuliwa dhidi yako ikiwemo kuondoka kwa nguvu.

IMETOLEWA LEO HII TAREHE 14/09/2020.
SCHOLASTIKA C. KEVELA
DALALI WA MAHAKAMA DODOMA.
NAKALA: 1.THE REGISTRED TRUSTEES OF NOOR MASJID DODOMA.
2.MWENYEKITI MTAA WA MADUKANI.
3.MTENDAJI KATA YA MADUKANI.

115907102

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglican Dayosisi ya Lweru – Muleba, Meshack E. Mwizagi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Land Cruiser Hardtop lenye namba za usajili **T 950 DDC** na Chasis namba **JTERB71J600078747** mali ya kanisa hilo. Ametoa taarifa polisi na kupewa RB namba **KAG/MUL/RB/631232/2020.**

115907402

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**GEORGE LUAMBANO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 936 APB** aina ya **TBETTER rangi** nyekundu.Chassis namba **LZEPCKLA9D6803738.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/677490/2020**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB:**
**+255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

# Mauaji Harusini-30

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango. (0716 350534)**

Sura ya Eddy ilionekana kubadilika. Mara nyingi akiongea maneno yenye mlengo ya kipelelezi, huwa hata sura yake inabadilika kiasi fulani.

Shani aliligundua hilo. Ndiyo maana wakati mwingine anamuona kama ni mtu wa ajabu kidogo.

"Sawa dereva, usiwe na wasiwasi na ikifika mwisho wa mwezi nikumbushe mshahara wako." Shani alizungumza kwa mzaha. Mzaha ambao ulimlainisha Eddy kutoka kwenye sura yake kikazi, na kurejea ile ya kawaida iliyozoeleka sana. Shani alifanya vile kwa makusudi ili kumuondoa kwenye hali ile.

Alijua kuwa mara nyingi Eddy ni mtu wa maneno ya mapenzi, mzaha, utani na ni kama komediani fulani hivi. Lakini cha ajabu kuna wakati anageuka na kuwa kama askari fulani hivi.

"Kwa wewe sitaki mshahara wa pesa, najua unazo tu, utanilipa." Alidakia Eddy.

"Sasa unataka nikulipe nini ambapo sina?"

Jibu hilo lilimfanya Eddy aangue kicheko.

"Mhh Shani siku hizi na wewe hujambo kwa maneno."

"Si umenifundisha mwenyewe."

"Na kweli. Tena vya kufundishwa huwa vinazidi,"

"Kweli kabisa."

"Sasa wewe ulitaka nikulipe nini?" Shani alirudi swali.

"Unilipe wewe." Ni jibu lililowafanya wapenzi hao wapya waange vicheko.

"Yaani Eddy wewe, sijakupatia mwezio, unajua wewe una vituko?"

"Kwani wewe uliponiuliza hilo swali, utarajia nikujibu nini?"

"Kwa hiyo nikulipe mimi."

"Wewe ndiyo."

"Haya nitakulipa."

"Hayo ndiyo maneno."

Alipomshusha kwake, Eddy alirudi nyumbani kwake Kijitonyama.


Hata hivyo akili yake ilimwambia kuwa itafika wakati itabidi awe naye.

Awe naye kama mpenzi wake, lakini pia ni kwa ajili ya ulinzi wake pia.

Aliwaza jinsi Shani alivyo mwenye furaha sana kwa sasa kwa ajili yake.

Na pia hajui chochote kuhusu kuwepo kwenye hatari. Hicho ndicho alichokuwa akikitaka Eddy.

Hakupenda msichana huyo aishi kwa hofu. Kuishi kiitelejensia awaachie wao kina Eddy.




*********************

"Hivi ninavyoawaambia Fikiri hayupo tena dunia." Jim alisema akiwaangalia ndugu zake kwa zamu.

"Ni kazi ya George. Japo ni mdogo kuliko wote hapa, lakini amefanya kazi kubwa sana."

Kilikuwa ni kikao kingine cha siri cha wanandugu hao. Lengo ni lile lile, kumuua Shani ili wagawane mali za marehemu baba yake, Patiyo.

"Ina maana tumeua ndege wawili kwa jiwe moja. Tayari Fikiri ameshafanya ile kazi ya kuweka sumu kwenye chakula cha Shani kwa shilingi milioni moja tu. Atakufa baada ya miezi mitatu mpaka minne hivi. Badala ya kutumia shilingi milioni moja nyingine kumpa Fikiri, tumetumia shilingi laki moja tu kummaliza." Jim alisema akitabasamu, tofauti na ingepaswa awe kwa kitu ambacho anakiongea.

"Ina maana George ndiye aliyemuua Fikiri?" Ben aliuliza.

"Hapana" George alidakia.

"Nilipofika maeneo ya Kigogo nilimpata kijana mmoja mvuta bangi hivi, nilikaa naye na kumpanga afanye mauaji hiyo. Aliyatekeleza kirahisi tu kwa kutumia kisu, baada ya kumnywesha gongo, na kumvutisha bangi na laki moja juu." Alijisifiia.

"Mnasikia ndugu zangu, kwa sasa siri imerudi kwetu. Fikiri kuendelea kuwa hai, ilikuwa ni hatari kwetu, yaani siku yoyote ile lingebumburuka, akikamatwa sisi tungekuwa tumekwisha." Jim aliendelea kuwapa somo ndugu zake.

"Yule mhuni aliyemuua Fikiri hajui chochote, yeye aliahidiwa pesa tu, lakini pia hamjui aliyepanga naye njama, yeye aliambiwa tu huyu mtu alitembea na mke wa mtu kwani hiyo kisasi kinahitajiwa."

Kwa kauli moja, waliridhika na mpango wao kabambe ambao waliupanga wa kumuua Shani, lakini wakisubiri baada ya miezi mitatu ili kuona matokeo ya sumu aliyokula.

***************************

"Unasikia Sherry, mimi ningependa uhamie kwangu."

Shani alimtazama Eddy kwa jicho la mahaba na tabasamu zito na kumjibu.

"Mhh, yaani mpenzi tayari umeshaanza kuwa na wivu? Kwa nini wakati tumeendelea kukaa kila mtu na kwake na umekuwa ukinipata kila unaponihitaji." Shani aliuliza.

Si kwamba Shani alikuwa hapendi kukaa kwa Eddy, lakini alikuwa anataka kujua kilicho ndani ya mwanaume huyo.

Kwake Eddy, pamoja na kumpenda Shani, lakini lengo namba moja lilikuwa ni usalama mwanamke huyo.

Alijua kabisa kuwa kama kuna watu walimtuma Fikiri kumtulia Shani kwenye chakula, anaweza pia kutumia mbinu nyingine za kummaliza.

Kutokana na hali hiyo aliamua yeye kuwa mlinzi wake. Alichukua jukumu la kumchukua asubuhi kumpeleka kazini na kwenda kumchukua. Wakati huo na yeye akienda kazini baada ya kumpeleka na kumchukua baada ya kutoka kazini.

Bado aliona haitoshi, kwani kutokana na uzoefu wake kwenye mambo ya kachero, alijua inawezekana kabisa muuaji akatumia fursa hiyo baada ya yeye kuondoka.

Kitu pekee ambacho kilimpa imani ni aina ya sumu aliyotakiwa aile kwenye chakula ni ya kuua taratibu.

Kutokana na uzoefu wa kazi yake alijua kabisa kuwa lengo la wauaji ni kwa kwamba Shani afe taratibu.

"Inawezekana kabisa wanasubiri baada ya miezi mitatu." Aliwaza.

Pamoja yote, bado akili ya kikachoro iliendelea kumwambia awe na tahadhari, kwani watu wanaoitafuta roho ya Shani bado wapo na wanafanya kazi mchana kutwa kuhakikisha msichana huyo haendelei kuwa duniani.

Ingekuwa rahisi tu kama angemwambia Shani kuwa kuna watu wanamtafuta ili wamuue, lakini alikuwa hataki kabisa kumwambia hilo.

"Ina maana Sherry, mimi kukwambia tukae wote nyumbani ni kosa?"

"Hapana nauliza tu."

"Basi kwa sasa ningependa kuwa karibu zaidi na wewe."

"Mhhh jamani, haya, mimi nimekubali.""Sawa lakini kwa muda kwanza."

"Hata moja kwa moja siyo mbaya, mimi ni wako tu."

"Hapana, baadaye nataka urudi nyumbani kwako, ili nifanye taratibu zinazotakiwa."

"Taratibu gani?"

"Si za kuoa."

Jibu hilo lilimtia ganzi Shani. Hakutegemea neno hilo kwa sasa kutoka kwa Eddy. Alivuta picha atakavyokuwa mke halali wa mwanaume huyo aliyetokea kumhusudu mno. Mtu aliyebadilisha maisha yake na kuwa na furaha na amani muda wote.

"Kweli utanioa Eddy?"

"Kama nisipokuoa wewe nikamuoe mwanamke gani mwingine. Si bora tu basi nikae bila kuona."

Majibu hayo yalimfanya Shani abubujikwe na machozi. Akamkumbatia Eddy. Alijihisi kama tayari amekuwa mke wake.

Ni kweli kabisa Eddy alikuwa amempenda kwa dhati Shani. Akili ya kumuoa ilikuwepo. Wakati Shani akidhani itakuwa ni kazi rahisi tu, mwenzake aliwaza kwanza jinsi ya kumaliza tatizo zito linalomzunguka Shani.

Tayari alikuwa amezima jaribio la kumuwekea sumu kwenye chakula. Lakini kabla ya kumuoa, alijua kuwa tukio zito linaandaliwa kwa ajili ya msichana yule kama watesi wake wakigundua kuwa yuko hai baada ya miezi mitatu kupita. Ni lazima waandae mpango mwingine wa kumuangaliza. Mpango gani? Wa sumu? Risasi? Kumtengenezea ajali? au kumteka. Wakati Eddy akiwa amekumbatiwa na Shani, akili yake iliwaza mengi.

"Ni lazima niwasake hawa watu kabla hawajafanya chochote juu ya mrembo huyu." Alijiambia

***Itaendelea Jumamosi***

# JUVENTUS

## YATHIBITISHA HIGUAIN KUONDOKA




**TURIN, Italia**

JUVENTUS imethibitisha kukatisha mkataba wake na Gonzalo Higuain na hivyo itawagharimu mabingwa hao wa Serie A, euro milioni 18.3 kama fidia.

Higuain mwenye umri wa miaka 32, alitua Juve kutoka Napoli mwaka 2016 na ameshinda mataji matatu ya Serie A na mawili ya Coppa Italia.

Fowadi huyo ambaye alitumia msimu wa 2018-19 akicheza kwa mkopo kule Milan na Chelsea, alifunga mabao 66 katika mechi 148 alizoichezea Juve.

Akiwa anahusishwa na mpango wa kwenda Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, MLS, kuondoka kwa Higuain kulithibitishwa na Juve Alhamisi.

Nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Argentina mkataba wake na Juve ulikuwa unamalizika mwaka 2021.

"Klabu ya Soka ya Juventus (S.p.A), inatangaza imefikia makubaliano ya kuvunja mkataba na mchezaji Gonzalo Gerardo Higuain," ilisomeka taarifa ya klabu hiyo.

Higuain amekuwa akihusishwa sana na kuhamia katika klabu inayomilikiwa na David Beckham, Inter Miami kwenye Ligi Kuu Marekani, sehemu ambayo mchezaji mwenzake wa zamani pale Juve, Blaise Matuidi anakuita nyumbani.

# SCHUSTER

## AITABIRIA MAKUBWA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona, Bernd Schuster, amesema anaiona klabu hiyo ikishinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu 2020-21.

Barca ilimaliza msimu uliopita bila taji lolote na nahodha wake, Lionel Messi akataka kuondoka kabla ya kubadili uamuzi ya kukaa pale Camp Nou.

Rais Josep Maria Bartomeu pia yupo kwenye presha kubwa baada ya Messi kuomba kuondoka klabuni hapo.

Huku Barca ikitarajiwa kuanza kampeni ya Ligi Kuu Hispania kwa kucheza dhidi ya Villarreal Septemba 26, mwaka huu, Schuster ameiambia Onda Cero: "Naiona Barca ikishinda taji la LaLiga.

"Naona wanaweza kufanya mabadiliko makubwa na naamini wana nafasi ya kubeba taji msimu huu," aliongeza Schuster ambaye pia amewahi kuichezea Real Madrid na kuwa kocha wake.

Ronald Koeman amepewa mikoba ya kuwa kocha mpya akichukua nafasi ya Quique Setien, ambaye naye alichaguliwa kuchukua nafasi ya Ernesto Valverde, Januari.

Barca iliachia taji la Ligi kwa wapinzani wao Madrid msimu uliopita na wakakumbana na kichapo cha mabao 8-2 kutoka kwa Bayern Munich kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika hatua ya robo fainali.

# Pochettino: Nina ndoto kuinoa Real Madrid

**MADRID, Hispania**

MAURICIO Pochettino amesema hakupata ofa yoyote ya kuwanoa miamba wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Barcelona, huku bosi huyo wa zamani wa Tottenham akisisitiza ana ndoto ya kuinoa Real Madrid.

Pochettino alikuwa akihusishwa na Barca baada ya kufukuzwa kwa Quique Setien kabla ya kuteuliwa kwa Ronald Koeman.

Raia huyo wa Argentina, Pochettino, ambaye aliondoka Tottenham Novemba, mwaka jana aliulizwa kuhusu uvumi wa Barca.

"Hawakunipa ofa ya kuinoa Barca," alisema akiiambia Cope na Marca. "Sikuona mawasiliano yoyote na rais Josep Maria Bartomeu.

"Nimekula nae mara kadhaa kwa sababu tuna urafiki wa miaka mingi, tangu mwaka 2009 wakati niliposaini Espanyol."

Pochettino alifungua mlango wa kuinoa Barca, ingawa awali alibainisha kwamba ni ngumu kwake kukubali kuinoa klabu hiyo ya Camp Nou kutokana na uhusiano alionao na Espanyol ambao wapizani wa jiji moja na Barcelona.

Hata hivyo, Pochettino amesema kwa sasa ndoto yake kubwa ni kuinoa Real Madrid siku moja."

## HABARI MICHEZO



# MOURINHO:

## NDOMBELE AMERUDI KWENYE UBORA

**LONDON, England**

TANGUY Ndombele sasa anaonekana kuwa kwenye kiwango chake bora baada ya kocha, Jose Mourinho kuelezea maendeleo ya raia huyo wa Ufaransa.

Ndombele mwenye umri wamiaka 23, alijiunga na klabu hiyo akitokea Lyon kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 64 mwaka jana, lakini alikumbana na wakati mgumu katika msimu wake wa kwanza pale London.

Ndombele alianza katika mechi 12 tu za Ligi Kuu England kwa msimu wa 2019-20, huku majeruhi yakichangia kushindwa kung'ara.

Uvumi ulitawala kuhusu majaliwa yake ya kukaa pale Tottenham huku akihusishwa na mpango wa kutua Juventus.

Lakini baada ya kufunga bao la kwenye ushindi wa 2-1 katika mchezo wa kuwania kufuzu Ligi ya Europa dhidi ya Lokomotiv Plovdiv juzi Alhamisi, Mourinho alizungumza kuhusu hali ya Ndombele na namna anavyoonekana kubadilika.

"Tanguy yupo kwenye hatua ya kuimarika zaidi," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari.

"Msimu uliopita hakuwa hivi. Msimu uliopita alikwama na hakuonyesha maendeleo yoyote. Lakini kwa sasa anafanya mazoezi vizuri sana.

"Amepona kutoka majeruhi na sasa naona kabisa ana nafasi kubwa ya kuimarika zaidi kwa kiwango chake."

## SUAREZ ATAPATA NAFASI ASIPOONDOKA - KOEMAN

**BARCELONA, Hispania**

LUIS Suarez bado atakuwa na nafasi kwenye kikosi cha Barcelona kama hataondoka pale Camp Nou kipindi hiki cha dirisha la usajili, amesema kocha, Ronald Koeman.

Straika huyo wa Uruguay, Suarez amekuwa akihusishwa na kuondoka kikosini hapo kutokana na Koeman kutaka kukifanyia marekebisho, baada ya kuchukua mikoba ya Quique Setien.

Ilitarajiwa kwamba fowadi huyo ataondoka kwenda kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus, ingawa dili hilo sasa limeripotiwa kwamba limeshindikana kwa sababu ya kutakiwa kuwa na hati ya kusafiria ya Italia.

Suarez hakuwapo kwenye kikosi cha Barca kilichocheza mehi ya kirafiki na Girona Jumatano ambapo walishinda 3-1, lakini Koeman amesisitiza hataachwa kwenye kikosi chake kama akishindwa kuondoka.

"Nimezungumza nae kuhusu hatima yake na sasa tunasubiria kuona kama ataondoka au atabaki, bado hatujui," amesema Koeman akiiambia TV3 baada ya ushindi dhidi ya Girona.

"Lakini tunaheshimu kila mkataba hapa na kama hatapata klabu na akabakia, atakuwa kama mchezaji yoyote kwenye kikosi chetu."

# Liverpool yajitosa kwa Sarr

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool imetoa ofa kwa Watford ili kumsajili nyota wake, Ismaila Sarr, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Ripoti zinasema kwamba, Watford wanataka angalau pauni milioni 36 ili kumwachia fowadi huyo mwenye umri wa miaka 22.

Sarr msimu uliopita alifunga mabao matano na kutoa pasi za mwisho nne katika mechi 28 za Ligi Kuu England.

Liverpool wanataka kuimarisha safu yao ya ushambuliaji ambayo inaongozwa na Mohamed Salah na Sadio Mane.

Kwa mujibu wa ripoti hizo, Sarr mwenyewe anashauku kubwa ya kwenda pale katika dimba la Anfield na inaelezwa uhamisho wake unaweza kukamilishwa ndani ya wiki ijayo.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA, BAYERN ZAINGIA VITANI

Ni katika vita ya kuwania saini ya beki chipukizi wa Ajax ambaye anatabiriwa makubwa kwenye siku...

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imetajwa kuwa kwenye mipango ya kumsajili beki wa kulia chipukizi na ghali, Sergino Dest, kutoka Ajax katika kipindi cha majira ya joto.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 19 amekuwa kwenye kiwango bora kwenye safu ya ulinzi kinachovutia duniani na Kocha, Ronald Koeman anamwona nyota huyo kama mrithi wa muda mrefu wa Nelson Semedo, ambaye hamhitaji tena.

Kwa mujibu wa taarifa iliyoandikwa kwenye ukurasa wa kwanza wa gazeti la Mundo Deportivo jana Ijumaa, kocha huyo wa Barca, Koeman ameonyeshwa kuvutiwa zaidi na staa huyo wa Ajax na anataka atue Nou Camp kipindi hiki cha majira ya joto mwaka huu. Alieleza kuwa klabu inajaribu kufanya mchakato wa kumuuza beki wa Timu ya Taifa ya Ureno, Semedo ili kupata fedha za kuongezea kumnunua beki huyo wa kulia.

Semedo anaamini alikuwa kwenye mpango wa wachezaji wanaouzwa na klabu hiyo kutokana na kuwa katika kikosi kilichoambulia kichapo cha aibu cha mabao 8-2 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

Wakala wa Semedo, Jorge Mendes, amekaririwa akisema amepokea ofa kutoka kwa klabu ambayo hakuwa tayari kuitaja inayomtaka beki huyo kwa dau la kati ya pauni milioni 36 na 45 na Barcelona inaangalia uwezekano wa kukamilisha mchakato huo.

Dest anatajwa kuwa ndiye mchezaji ghali ambaye alikuwa kwenye orodha hiyo ya kuuzwa kutokana na uwezo wake wa kiufundi wa kukaba na kushangilia.

Pia anaweza kucheza nafasi zote za ulinzi kama itahitajika kupangwa.

Hata hivyo, Barcelona itakutana na ushindani kutoka kwa Bayern Munich katika kuwania saini ya beki huyo, ambao pia wanahitaji kujiimarisha kwenye safu ya beki wa kulia katika kipindi hiki cha majira ya joto.

Imeelezwa kuwa Bayern iliwasilisha ofa ya thamani ya chini ya pauni milioni tisa ambayo imekataliwa na vigogo hao wa Uholanzi.

Inaelezwa kuwa Ajax wanahitaji kulipwa kati ya pauni milioni 13 na pauni milioni 18 kumuuza beki huyo mwenye umri wa miaka 19, ambaye alizaliwa Uholanzi lakini anaichezea Timu ya Taifa ya Marekani.

Taarifa nyingine zinasema Barcelona inahitaji kumsajili Dest kwa mkataba wa mkopo wa mwaka mmoja lakini kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja wakati wa majira ya joto mwakani.

Beki huyo ameichezea Ajac mechi 36 katika mashindano yote na kufunga mabao mawili wakati akitengeneza pasi za mwisho za mabao sita.

Barca inatajwa pia inawinda saini za nyota wa Arsenal, Hector Bellerin na Joao Cancelo wa Manchester City lakini klabu zote za Ligi Kuu England zimesisitiza wachezaji hao hawauzwi.

## KWA UFUPI

**SARR ANUKIA LIVERPOOL**

LIVERPOOL imeonyesha nia ya kumhitaji, Ismaila Sarr kutokana na nafasi aliyokuwa nayo kwenye kikosi cha Watford. Thamani ya straika huyo wa Timu ya Taifa ya Senegal mwenye umri wa miaka 22 ni pauni milioni 36. ***(Mail)***

**PERISIC, COMAN SOKONI**

MANCHESTER United imejipanga kumsajili winga wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Croatia, Ivan Perisic (31), winga Mfaransa wa Bayern Munich, Kingsley Coman (24) na Mbrazil, Douglas Costa kutoka Juventus ambaye ana umri wa miaka 30. ***(ESPN)***

**KHEDIRA KUTUA UNITED**

MABOSI wa Manchester United wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Sami Khedira (33), baada ya mkataba wake na Juventus kumalizika. ***(Sun)***

**MENDY RASMI CHELSEA**

WAKALA wa golikipa wa Rennes na Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy, amesema tayari wameshafikia makubaliano ya nyota huyo kutua kwenye kikosi cha Chelsea. ***(Stades via Star)***

**CHELSEA WAMFUATA RICE**

CHELSEA inajiandaa kuwasilisha ofa ya kumwania kiungo wa West Ham na Timu ya Taifa ya England, Declan Rice (21), ambaye atakuwa mchezaji wa mwisho kutua klabuni hapo endapo mchakato wa kumsajili utafanikiwa. ***(Simon Phillips via Express)***

**ARSENAL YAKWAMA**

KLABU ya Brentford imekataa kupokea ofa ya pauni milioni 10 kutoka kwa Arsenal ambao wanahitaji kumsajili golikipa Mhispania, David Raya, mwenye umri wa miaka 25. (Telegraph)

**SPURS KUMKOSA INGS**

MABOSI wa Southampton wameiambia Tottenham kuwa straika, Danny Ings, ambaye ana umri wa miaka 28, hauzwi kwa dau lolote la fedha. ***(Mail)***

**UNDER KITAELEWEKA**

LEICESTER City inakaribia kukamilisha usajili wa mkopo wa straika wa Timu ya Taifa ya Uturuki, Cengiz Under kutoka Roma, wakati beki wa Burnley, James Tarkowski (27), bado anatajwa kutakiwa na Kocha wa Foxes manager Brendan Rodgers. ***(Sky Sports)***

**CLYNE ANUKIA PALACE**

BEKI wa zamani wa Liverpool ambaye kwa sasa ni mchezaji huru, Nathaniel Clyne (29), anafanya mazoezi katika kikosi cha Crystal Palace na huenda nyota huyo raia wa England, akapewa mkataba wa kuitumikia klabu hiyo. ***(Standard)***

**DZEKO KUTUA JUVENTUS**

EDIN Dzeko anajiandaa kujiunga na Juventus kwa mkataba wa miaka miwili akitokea Roma. Uhamisho wa straika huyo wa Bosnia na Herzegovina unamaanisha kuwa mchakato wa Luis Suarez kuondoka Barcelona na kwenda kwa mabingwa hao wa Serie A utakufa. ***(Goal)***

**ARSENAL, AOUAR SAFI**

ARSENAL imefikia makubaliano binafsi na kiungo Mfaransa wa Lyon, Houssem Aouar, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Star)***

**PSG, INTER ZAMWANIA ALLI**

KIUNGO wa Tottenham na Timu ya Taifa ya England, Dele Alli, ambaye ana umri wa miaka 24, ametajwa kuwindwa na klabu za Paris St-Germain na Inter Milan. ***(Mail)***

**JOVIC KUONDOKA MADRID**

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Serbia, Luka Jovic (22), anajiandaa kuondoka katika kikosi cha Real Madrid. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# RASMI SIMBA SC, YANGA KUIFUATA AZAM CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA na Yanga msimu huu zitalazimika kucheza mechi zao ugenini dhidi ya Azam FC kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliioko Chamazi jijini Dar es Salaam baada ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuridhia timu hiyo kutumia uwanja wake wa nyumbani dhidi ya vigogo hao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), Almasi Kasongo, alisema Azam FC itatumia uwanja wa Azam Complex ikiwa mwenyeji dhidi ya Simba na Yanga kutokana na uwanja wao kuwa na vigezo kamili.

Kasongo alisema uwanja wa Azam Complex unakidhi vigezo vilivyowekwa na watahakikisha wanazingatia idadi sahihi ya mashabiki watakaoingia uwanjani.

"Sio tumepokea ombi lao, ila ni wazi Azam FC msimu huu watatumia uwanja wao kwa sababu una sifa zilizowekwa kutumika michezo ya Ligi Kuu, unakidhi sifa," Kasongo alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema waliliandikia barua TFF kuhusu kutumia uwanja wao katika mechi zao nyumbani.

Popat alisema tangu msimu uliopita walikuwa wameshaamua kurudisha mechi hizo Chamazi, lakini kilichokwamisha ni ukarabati wa uwanja ambao ulikuwa haujakamilika.

"Msimu huu tumejipanga kwa sababu mwanzo, Simba na Yanga zilikuwa zinacheza kwenye uwanja huu, lakini tulisitisha kutokana na matatizo ya mashabiki, lakini kwa sasa tumejipanga kwa ulinzi, hasa maeneo ya chooni ambako kulikuwa na matatizo sana," alisema Popat.

Mara ya mwisho kwa Azam kutumia uwanja wake wa Azam Complex kucheza na timu za Simba na Yanga ilikuwa ni msimu wa Ligi Kuu 2017/18, lakini walirejea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru, baada ya kile kilichodaiwa kutokea uharibifu kwenye uwanja huo.



Mkufunzi wa Kimataifa wa Fifa, Dk. Henry Tandau (kushoto), akitoa maelekezo katika semina ya Uongozi na Utawala wa Soka ya Wanawake inayoendelea jijini, Dar es Salaam. **PICHA : TFF**

# Kabunda atamba kumfunika Kagere

**Na Adam Fungamwango**

WINGA machachari wa KMC, Hassan Kabunda, amesema anatarajia kufunga mabao mengi katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaoendelea kwa sababu amerejea kwenye kiwango chake cha juu.

Akizungumza na gazeti hili, Kabunda alisema anataka kuisaidia timu yake ifanye vizuri msimu huu na yeye akiwa kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu.

Kabunda alisema ili kufikia 'ndoto' hizo, anahitaji ushirikiano kutoka kwa wenzake na anashukuru msimu huu wameanza vema kwa kushinda mechi mbili za kwanza.

"Msimu huu nimejipanga, nimejipanga kufunga magoli mengi, tena nimepania kufunga kila mechi, labda itokee bahati mbaya tu," alisema Kabunda ambaye ni mtoto wa beki wa zamani wa Tukuyu Stars na Yanga, Salum Kabunda 'Ninja'.

Winga huyo ambaye alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu alipokuwa Mwadui kiasi Simba na Yanga kuanza kumfukuzia, hakuwa kwenye kiwango kilichozoeleka na KMC.

Msimu wa kwanza alipojiunga 2018/19, alimaliza akiwa na mabao matatu tu, huku uliopita alimaliza ligi akiwa magoli mawili ambayo msimu huu ameyapata ndani ya mechi mbili alizocheza.

Kabunda amefunga goli moja katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mbeya City na lingine walipoondoka na pointi tatu baada ya kuwafunga Tanzania Prisons magoli 2-1.

## Morris kuikosa Mbeya City

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Azam FC kilitua salama jijini Mbeya jana tayari kuwakabili wenyeji Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine, lakini kikiwa bila ya beki wake mkongwe, Agrey Morris ambaye ni majeruhi.

Msemaji wa Azam FC, Thabit Zakaria, alisema jana msafara wa timu hiyo umeondoka na wachezaji 24, pamoja na viongozi tisa.

Kiongozi huyo alisema jana asubuhi wachezaji wake walifanya mazoezi ya mwisho kabla ya kuanza safari hiyo na kuongeza wanakwenda kucheza kwenye uwanja ambao wana uzoefu nao.

Naye Kocha Mkuu wa timu hiyo, Aristica Cioaba, alisema wachezaji wake wapo tayari kwa ajili ya kupambana na Mbeya City na wanaupa 'umuhimu mkubwa' mchezo huo wa ugenini.

Cioaba alisema lengo lao ni kupata pointi tatu na anawaomba mashabiki wa timu hiyo waliopo jijini humo wajitokeze kwa wingi kuwaunga mkono.

"Lengo langu ni kupata pointi tatu ili nishike nafasi ya juu katika msimamo wa ligi, ninawaheshimu wapinzani wetu na tunaiona ni mechi muhimu sana kwetu, nasikitiza tutamkosa Agrey," alisema Cioaba.

Daktari wa timu hiyo, Mwanandi Mwankemwa, alisema Agrey alipata mshtuko wa msuli mbele ya nyonga katika mechi dhidi ya Coastal Union na hivyo amepewa siku tano za mapumziko.

## Usajili wachezaji Z'bar wasogezwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza kusogeza mbele muda wa kukamilisha mchakato wa usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu wa 2020/21 hadi kufikia Septemba 30, mwaka huu.

Awali ZFF ilitangaza mwisho wa kukamilisha mchakato wa usajili ni leo Septemba 19, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Mohammed Ameir, alisema sababu ya kusogeza mbele dirisha hilo la usajili ni kuzipa nafasi klabu vyote kukamilisha usajili wao kwa utulivu kutokana na kuchelewa kumalizika kwa ligi zao.

Ameir alisema asilimia kubwa timu zinazoshiriki Ligi za Ngazi ya Mikoa ya Wilaya, zimemaliza ligi zao ndani ya wiki hii huku vilabu vichache ndio vilivyokamilisha mchakato huo kwa wakati.

"Kama inavyojulikana msimu wa 2019/20 ulikuwa msimu mbaya, ligi za ZFF zilianza Juni baada ya kuruhusiwa na serikali ,huku ligi za madaraja mengine zilianza Agosti, hivyo vilabu vilikuwa havina pumzi ndio maana ZFF tukaona tusogeze mbele usajili ili hizi siku 10 zilizoongezwa zisaidie kumaliza usajili kabla ya dirisha halijafungwa,"alisema.

Kiongozi huyo amezipongeza timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kwa kufanya usajili wao kwa wakati.

# Michezo

Jumamosi Septemba 19, 2020

Nipashe




## BARCA, BAYERN ZAINGIA VITANI

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (kulia), akiwania mpira dhidi ya kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Bernard Morrison katika mazoezi ya kujiandaa kuikaribisha Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho jijini, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

## KAGERE AANDALIWA KUONGOZA 'MAUAJI'

**Na Saada Akida**

NJAA ya mabao ndio kiu kubwa ya Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ambaye ameonekana hana masihara kwa washambuliaji wake baada ya juzi kuwapa mbinu mpya za kufunga kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Katika mazoezi hayo ambayo Nipashe ilishuhudia, Mnyarwanda, Meddie Kagere, alionekana kuongoza washambuliaji wenzake katika mazoezi ya kufunga ikiwa ni malengo ya Sven kuona kikosi chake kinapata ushindi mnono katika mechi hiyo inayofuata.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana mara baada ya mazoezi ya asubuhi, Sven alisema amekiandaa vizuri kikosi chake na atahakikisha wanatumia vema uwanja wa nyumbani kwa kupata ushindi.

Sven alisema wachezaji wake wapo fiti na tayari kwa ajili ya kuondoka na matokeo mazuri ambayo yatawaweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi.

"Ni mechi ya ushindani, mechi iliyopita uwanja haukuwa rafiki na sasa tumerudi nyumbani kuhakikisha tunapata matokeo mazuri. Kuhusu mfumo naweza kutumia 4:4:2 huku Kagere akianza, inategemea na mpinzani wetu tunayekutana naye, kikubwa ni kupata matokeo mazuri katika mechi yetu ya Jumapili," alisema Sven.

Kocha huyo alisema mechi iliyopita hawakuwa na matokeo mazuri sababu ya uwanja kutokuwa rafiki lakini sasa wamejipanga kutumia vema uwanja wa nyumbani.

## WEST BROM YAJITOSA KUMWANIA SAMATTA

**LONDON, England**

WEST Brom imeanza mchakato wa kunasa saini ya mshambuliaji, Mbwana Samatta kutoka kwa majirani zao, Aston Villa ambaye pia anawaniwa na klabu ya Uturuki.

Slaven Bilic anataka kumsajili nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), mwenye umri wa miaka 27, ambaye yuko katika mazungumzo ya kujiunga na Fenerbahce.

West Brom inahitaji kumsajili Samatta kwa mkopo au kumnunua endapo dau lake litakuwa la kawaida, wakati Villa tayari wameshaonyesha nia ya kumruhusu kuondoka klabuni hapo.

Fenerbahce inatajwa kukaribia kukamilisha mazungumzo na nyota huyo lakini Albion inaamini inaweza kumpata Samatta kutokana na ofa itakayomwekea mezani.

Samatta alijunga na kikosi cha Dean Smith akitokea Genk kwa dau la pauni milioni 9.1 Januari, mwaka huu kwa mkataba ambao utamalizika ifikapo 2024.

# YANGA, KAGERA SUGAR VITA VYA REKODI, POINTI

### Carlinhos kila kona Bukoba, kila timu yatambia usajili, Maxime dakika 90, Zlatko kumpiku Eymael leo?...

**Na Isaac Kijoti, BUKOBA**

WAKATI Kagera Sugar ikiikaribisha Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Kaitaba mjini hapa leo, vita kubwa itakuwa ya kuwania rekodi na pointi tatu muhimu huku makocha, Mecky Maxime na Zlatko Krmpotic wataziongoza timu zao katika mchezo huo wa raundi ya tatu.

Mbali na kupata pointi ambacho ndicho kitu cha muhimu kwa kila timu leo, Zlatko atashusha kikosi chake uwanjani akitaka kufuta rekodi mbaya ya mtangulizi wake, Mbelgiji Luc Eymael ambaye mchezo wake wa kwanza dhidi ya Kagera Sugar katika uwanja huo alikubali kipigo cha mabao 3-0 msimu uliomalizika.

Ilikuwa ni Januari 15, mwaka huu wakati Yusuph Mhilu, Ally Ramadhani na Peter Mwalyanzi walipopeleka kilio cha mabao 3-0 kwa Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita wakati ikinolewa na Eymael, hivyo Zlatko atataka kuandika rekodi mpya ya kutokubali kipigo lakini pia kuondoka na alama tatu muhimu.

Lakini pia kwa Kocha wa Kagera Sugar, Maxime, atakuwa akiwania kuendeleza ubabe huo dhidi ya Yanga akiwa nyumbani huku pia akitaka kulipa kipigo cha bao 1-0 walichokipata katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu msimu uliopita timu hizo zilipokutana Uwanja wa Mkapa Julai 8, mwaka huu bao likifungwa na Mghana Bernard Morrison ambaye kwa sasa anawachezea mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba.

Tayari makocha na viongozi wa benchi la ufundi wa timu hizo kila mmoja ameelezea matumaini yake ya kufanya vizuri kuelekea mechi hiyo itakayoanza saa 10: 00 alasiri.

Kwa upande wa Maxime, amesema kikosi chake kimejiandaa vizuri kuibuka na ushindi katika mechi hiyo ya leo na hahofii usajili mkubwa wa wapinzani zao kwa kuwa hata Kagera Sugar imefanya usajili mzuri msimu huu.

"Wachezaji wote wapo salama na maandalizi yamefanyika vizuri, siku zote timu inapojiandaa vizuri inahitaji pointi, tumesajili vizuri tunauhakika wakufanya vizuri," Maxime alisema.

"Tusubiri dakika 90, lakini naamini utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote, hivyo mashabiki wajitokeze kwa wingi kuja kuipa sapoti timu yao."

Meneja wa Yanga, Hafidh Saleh, akizungumzia maandalizi ya timu hiyo, alisema wamesafiri na jumla ya wachezaji 20 na wote wapo tayari kwa mchezo huo, hivyo ni jukumu la kocha kuamua aanze na nani.

Saleh alisema wanatarajia utakuwa mchezo mgumu kwa pande zote, lakini wamejipanga kuvuna pointi tatu kwa kuwa lengo lao msimu huu ni kutwaa ubingwa wa ligi hiyo.

"Kagera Sugar si timu ya kuibeza hata kidogo, tunajua utakuwa mchezo mgumu, lakini tumefanya maandalizi mazuri na wachezaji wote wapo fiti kwa mchezo na wana ari ya kufanya vizuri, tusubiri tuone," alisema meneja huyo.

Kuhusu majeruhi, meneja huyo alisema mbali na Mapinduzi Balama, wachezaji wote wapo fiti na wale ambao hawakusafiri na timu, wanaendelea na mazoezi jijini Dar es Salaam.

Yanga ambayo ilitua mjini hapa kwa ndege juzi saa 3:30 asubuhi, tangu ametua kiungo wa timu hiyo, raia wa Angola, Carlos Carlinhos ndilo jina ambalo limekuwa likitajwa na kusifiwa zaidi na mashabiki wa timu hiyo mjini hapa.

Kila mmoja amekuwa akitamani kuona akianzishwa katika kikosi cha kwanza kitakachoanza leo, lakini bado uamuzi huo unabaki chini ya Zlatko ambaye awali aliliambia Nipashe kuwa mchezaji huyo bado hajawa fiti kutosha kucheza kwa dakika zote 90 za mchezo, hivyo ataendelea kupata muda mchache dimbani sambamba na mshambuliaji, Sogne Yacouba, raia wa Burkina Faso.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela alisema: "Msimu huu tumesajili vizuri na tunamatumaini ya kushinda kwa kuwa lengo letu msimu huu ni kutwaa ubingwa."

Wachezaji wa Yanga ambao hawakusafiri na timu mbali na Balama ni pamoja na Paul Godfrey, Juma Mahadhi, Abdallah Shaibu 'Ninja' na kipa Farouk Shikalo. Mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa leo ni kati ya 'Maafande' wa Tanzania Prisons dhidi ya Namungo FC kutoka Lindi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >